

**MCHANGO WA SAJILI YA KIDINI KATIKA KUFANIKISHA RIWAYA
MBILI ZA KEN WALIBORA (*KIDAGAA KIMEMWOZEA NA NDOTO YA
ALMASI*)**

PHANICE MARISYA

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA IDARA YA KISWAHILI, CHUO
KIKUU CHA NAIROBI**

2017

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu chochote kingine.

Sahihi.....

Tarehe.....

Phanice Marisya

(Mtahiniwa)

Kazi hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi.....

Tarehe.....

Dkt. Evans Mbuthia

(Msimamizi)

Sahihi.....

Tarehe.....

Dkt.Obuchi Moseti

(Msimamizi)

YALIYOMO

Ungamo.....	ii
Yaliyomo.....	iii
Tabaruku	vi
Shukrani	vii
Ikisiri.....	viii

SURA YA KWANZA

1.1 Usuli wa mada.....	1
1.2 Tatizo la utafiti	4
1.3 Madhumuni ya utafiti.....	6
1.4 Maswali ya utafiti	6
1.5 Sababu za kuchagua mada hii.....	6
1.6 Upeo na mipaka ya utafiti	7
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii.....	8
1.8 Msingi wa kinadharia.....	12
1.8.1 Kubanika kwa neno.....	14
1.8.2 Kupanuka kwa neno.....	15
1.8.3 Kukisia kwa neno	17
1.9 Mbinu za utafiti.....	19
1.10 Hitimisho	20

SURA YA PILI

UDHIHIRIKAJI WA SAJILI YA DINI YA KIKRISTO KATIKA RIWAYA ZA *KIDAGAAA KIMEMWOZEA NA NDOTO YA ALMASI*

2.1 Utangulizi	22
2.2 Msamiati wa kipekee	23
2.2.1 Msamiati unaotaja Mungu na Yesu.....	23
2.2.2 Msamiati unaotaja majina ya watu yanayopatikana katika Biblia	24
2.2.3 Msamiati uliosheheni sifa kwa Mungu	26
2.3 Lugha yenye matumaini.....	26
2.4 Kudondoa kauli kutoka katika Biblia	28
2.5 Lugha iliyosheheni sifa.....	29

2.6 Lugha yenye unyenyekevu	29
2.7 Matumizi ya tamathali za usemi	31
2.7.1 Jazanda/Mafumbo	32
2.7.2 Sitiari	34
2.8 Lugha yenye heshima	34
2.9 Hitimisho	36

SURA YA TATU

UFASIRI YA SAJILI YA DINI YA KIKRISTO

3.1 Utangulizi	38
3.2 Kupanuka kwa neno	39
3.2.1 Vita	40
3.2.2 Enda.....	41
3.2.3 Dada	41
3.2.4 Nishauriane	42
3.2.5 Osha	42
3.2.6 Kutembea na Yesu	43
3.2.7 Mungu ni mkubwa	44
3.2.8 Mungu ameniambia.....	44
3.2.9 Ngo'a macho	45
3.2.10 Kuona pila macho hiyo kapisa	45
3.2.11 Kusafisha njia	46
3.3 Kubanwa kwa neno.....	47
3.3.1 Ndugu.....	48
3.3.2 Baba	48
3.2.3 Bwana.....	48
3.3.4 Neno	49
3.3.5 Kukubalika	49
3.4 Kukisia maana	50
3.5 Hitimisho	51

SURA YA NNE

MCHANGO WA SAJILI YA DINI YA KIKRISTO KATIKA RIWAYA ZA *KIDAGAA KIMEMWOZEA NA NDOTO YA ALMASI*

4.1 Utangulizi.....	52
4.2 Maudhui	53
4.2.1 Dini	53
4.2.2 Unafiki	54
4.2.3 Mabadiliko	55
4.3 Ukuzaji wa dhamira	56
4.4 Ukuzaji wa wahusika	58
4.4.1 Mama	59
4.4.2 Masasi.....	61
4.4.3 Mtemi Nanasa Bora	62
4.4.4 Balozi	63
4.4.5 Babake Nasaba Bora	63
4.5 Kujenga uhalisia.....	64
4.6 Kuendeleza msuko.....	65
4.7 Hitimisho.....	65

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi.....	67
5.2 Muhtasari wa kazi	67
5.3 Hitimisho	68
5.4 Mapendekezo	68
MAREJELEO	69

TABARUKU

Natabarukia kazi hii wazazi wangu, Bwana Gideon Aliongo na Bi. Esther Asande Aliongo kwa kunipa msingi wa elimu ulioniwezesha kuendeleza masomo yangu hadi kiwango hiki.

SHUKRANI

Ashukuriwe Mwenyezi Mungu kwa rehema na baraka zake katika kazi hii. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Evans Mbuthia na Dkt.Obuchi Moseti kwa kutwaa wakati wao kuniongoza, kunishauri na kunitia moyo katika hatua zote za utafiti wangu.

Zaidi ya hayo, nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili: Prof. John Habwe, Prof. Iribemwangi, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Hezron Mogambi, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Jefwa Mweri, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatia, Dkt. Zaja Omboga na Bw. Gichobi Mungania. Pokeeni shukrani zangu kwa kunihimiza wakati wa kufanya kazi hii.

Shukrani zangu pia ziwaendee wasomi wenzangu ambao ni pamoja na Magdalene Kanda, Julita Wanjala, Zani Mwazani, Eveline, Lidya Shaviya, Paul Sito, Gladys Kinyua, Daina Sungu, Lawrence Orange, Florence, Queen Ndoni, Damarice Otuoma na Hudson Nyandiwa. Safari hii ya masomo ya shahada ya uzamili haingekamilika pasipo msaada wenu.

Sina budi kuwashukuru wazazi wangu Bwana Gideon Aliongo na Bi. Esther Asande Aliongo kwa kujitolea kwa udi na uvumba ili kuhakikisha kuwa nimepata msingi wa elimu bora.

Mwisho na muhimu sana namshukuru mume wangu Wycliffe Aluvara Imbwaga kwa kujitolea kwa hali na mali kunihimiza kuendelea na utafiti huu kila alipoona nikififia katika jitihada zangu za kuitekeleza shughuli hii. Naomba Mungu akufikishie heri na akuepushe na mabaya.

IKISIRI

Tuliamua kuchunguza jinsi mwandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* ametumia lugha ya kipekee anaporejelea masuala ya dini ya Kikristo ili kubainisha: sifa za sajili ya dini ya Kikristo zinavyojitokeza, michakato ambayo huwawezesha wafuasi wa dini ya Kikristo na wasomaji *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* kufasiri lugha inayohusiana na dini ya Kikristo kisha kuonyesha mchango wa matumizi ya sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya hizi. Katika uchunguzi wetu tuliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika. Nadharia ya pragmatiki leksika iliasisiwa na Blutner katika mwaka wa 1990. Katika nadharia hii alionyesha jinsi maana ya neno kiisimu ilibadilishwa katika matumizi. Yaani maana ya neno hufasiriwa kulingana na muktadha fulani wa matumizi. Katika uchunguzi wetu ilibainika kuwa sifa za sajili ya dini ya Kikristo zinadhahirika katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*. Baadhi ya sifa hizi ni kama vile msamiati unaosifu Mungu, matumizi ya mafumbo na nyimbo za kusifu Mungu. Pia tulionyesha kuwa sajili ya dini ya Kikristo imemwezesha mwandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* kufanikiwa katika kujenga maudhui, dhamira na wahusika miongoni mwa mambo mengine. Katika sura ya kwanza tumeangazia utangulizi wa kijumla kuhusu mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu ya kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti wetu, maswali ya utafiti, msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti. Katika sura ya pili tumeonyesha udhahirikaji wa wa sajili ya dini ya Kikristo katika matini husika. Aidha, tumeshughulikia uchanganuzi wa semi za dini ya Kikristo katika sura ya tatu huku tukiegemea kwenye kategoria za kimsingi zilizofafanuliwa na Wilson (2003) na Cartson (2002) katika nadharia ya pragmatiki leksika. Sura ya nne inahusu umuhimu wa sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya husika. Hatimaye tumehitimisha kazi hii na kutoa mapendekezo yetu katika sura ya tano.

SURA YA KWANZA

1.1 Usuli wa mada

Waandishi wengi wa kazi za kisanaa hutumia mbinu anuai za lugha ili kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu. Mbinu hizi humwezesha mtunzi wa kazi yoyote ile kuwasiliana na hadhira yake kwa njia mwafaka. Mbinu hizi mbalimbali za lugha anazotumia mtunzi wa kazi ya kisanaa ndizo zinaifanya fasihi kuitwa ‘sanaa’ kwa kuwa inatumia lugha kwa njia ya kipekee.

Tafiti anuai zimewahi kufanywa kuhusu mbinu mbalimbali watumiazo waandishi wa kazi za fasihi kuwasilisha ujumbe wao au kuyafikia malengo yao. Mbinu hizi hujumuisha uchunguzi wa istilahi za kifasihi miongoni mwa mbinu zingine tofauti. Hata hivyo, ni sharti ikumbukwe kuwa kila mtunzi wa kazi yoyote ya kifasihi huangazia masuala yanayohusu jamii mahususi. Mbali na kila msanii kutumia mbinu mbalimbali za lugha katika kazi yake, hana budi kudhihirisha upekee wa lugha anaporejelea miktadha mbalimbali ya jamii husika. Kila muktadha wa kijamii unafaa kumchochea mtunzi wa kazi ya fasihi kutumia lugha ya kipekee.

Kutokana na hali hii tulichagua mada ya kuchunguza jinsi mwandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* alivyotumia lugha ya kipekee anaporejelea masuala ya dini ya Kikristo na jinsi hali hii ilivyofanikisha uwasilishaji ujumbe wake. Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*, mwandishi ametumia lugha ya kipekee anapoyarejelea masuala ya dini ya Kikristo kama vile kutaja majina ya Mungu pamoja na kunukuu vifungu kutoka kwenye Biblia.

Kimsingi, mada tuliyochagua inahusu mchango wa sajili ya dini ya Kikristo katika kufanikisha riwaya mbili za Ken Walibora. Katika uchunguzi huu, tulijikita kwenye nadharia ya pragmatiki leksika. Jambo muhimu katika utafiti wetu ni kuchunguza umuhimu wa sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*.

Nadharia ya pragmatiki leksika inahusu maana katika muktadha. Yaani ufasiri wa kile watu wanasema katika muktadha mahususi na jinsi muktadha huathiri ufasiri wa ujumbe unaosemwa. Pragmatiki leksika ni nadharia ya vitendo. Hii ina maana kuwa nadharia hii huonyesha lugha inavyotumiwa katika muktadha maalum.

Lugha itumikayo katika muktadha wa kidini husheheni ushawishi fulani ambao huwafanya wahusika kufuata mkondo fulani wa kidini. Wahubiri anuai wa kidini hujaribu kila mbinu kuwateka kisaikolojia wafuasi wa dini husika. Jambo hili hutekelezwa kwa kutumia lugha maalum yenye ushawishi ili kuwachochea wafuasi wa dini husika kufuata imani mahususi za kidini.

Lugha itumikayo na viongozi wa dini ya Kikristo pamoja na maandishi katika vitabu vya kidini husheheni ushawishi, onyo na kwa kiwango fulani vitisho. Lugha hii huwapa wafuasi msukumo wa kufuata imani zinazoambatana na dini husika. Kwa mujibu wa Yule (1996), lugha hutumika kama chombo cha kupashiana ujumbe na hisia.

Sajili kama mitindo mbalimbali ya kutumia lugha huwa ni zao la miktadha na hali anuai katika jamii ambayo huathiri jinsi lugha hutumika. Kila jamii ina kaida ambazo hutawala

matumizi ya lugha. Kaida hizi ndizo husababisha kuwepo kwa mitindo mbalimbali ya lugha iitwayo sajili. Mukhwana (2011), anasema kuwa sajili katika taaluma ya Isimujamii humaanisha kaida na mikondo ya kimawasiliano itumiwayo katika hali na miktadha fulani fulani kwa madhumuni maalum.

Habwe na wengine (2010) wanasema kuwa ili kukidhi haja ya mawasiliano, makundi ya kijamii huibua mitindo na istilahi zinazowawezesha kurejelea shughuli za kikundi husika. Kila kundi la watu katika nyanja tofauti tofauti za maisha huwa na mtindo wake wa kutumia lugha ili kuafiki hali na majukumu fulani. Wafuasi wa dini ya Kikristo hutumia lugha katika upekee wake ili kufikia lengo la kuwashawishi watu kufuata mkondo maalum wa kidini. Kwa mujibu wa Fishman (1968), jamii ni muhimu kuliko lugha na kwamba jamii ndiyo hutuwezesha kupata muktadha ambao hutusaidia katika kuamua aina ya lugha itakayotumiwa.

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanasema kuwa dhana ya sajili iliasisiwa na mwanaisimu Halliday mnamo mwaka wa 1960 akiwa akifuatilia yale yaliyotajwa na waliomtangulia, hasa Firth katika miaka ya 1950. Ni bayana kuwa hali tofauti tofauti za kimuktadha katika jamii huathiri namna lugha hutumika. Halliday, M. A. na Hassan, R.(1976) wanasema kuwa muktadha wa hali ni vipengele vinavyotokea nje ya matini ambavyo vinatumia kubaini kama usemi uliotolewa ni mwafaka kwa mujibu wa uhalisi wa muktadha husika. Kwa kawaida, jamii huathiri matumizi ya lugha. Kuna vigezo mbalimbali katika jamii kama vile muktadha, hali, umri wa wazungumzaji na kadhalika ambavyo huathiri namna lugha hutumika. Kwa vile fasihi ni zao la jamii, mtunzi wa kazi

za fasihi hana budi kudhihirisha upekee wa lugha anapoangazia masuala na miktadha mbalimbali ya kijamii.

1.2 Tatizo la utafiti

Tafiti nyingi zimewahi kufanywa kuhusu mbinu mbalimbali za lugha ambazo watunzi wa kazi za kisanaa hutumia ili kuwasilisha ujumbe wao. Suala la sajili katika kazi za kisanaa halijashughulikiwa kwa upana. Hatuna budi kukumbuka kuwa fasihi inaihusu jamii na kwamba kila mtunzi wa kazi ya fasihi anafaa kuiangazia miktadha mbalimbali ya kijamii katika kazi yake. Hali hii ni muhimu kwani huifanya kazi ya kisani kuonekana halisi. Kutokana na ukweli kwamba kila msanii hujitahidi ili kuhakikisha kuwa kazi yake inaoana na hali halisi za kimuktadha katika jamii, tuliamua kuchunguza jinsi mwandishi anatumia lugha ya kipekee anaporejlea masuala ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*. Katika uchunguzi wetu tulibainisha: sifa za sajili ya dini ya Kikristo zinavyojitokeza, michakato ambayo inaiwezesha hadhira ya *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* kufasiri lugha inayohusiana na dini ya Kikristo na kuonyesha mchango wa matumizi ya lugha ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*.

Dini ni kiungo muhimu kwa binadamu. King'ei (1992) anasema kuwa lugha ya kidini huathiriwa kwa kiwango kikubwa na utamaduni ulioizaa dini ile. Kila dini ina utamaduni wake unaoifanya kuwa ya kipekee katika kuendeleza shughuli zake. Utamaduni unaweza kuelezwa kama mambo ambayo wanajamii huwa na makubaliano kuyahusu hivi kwamba yanajitokeza kama sheria zisizoandikwa. Dini hufungamanishwa na jamii kwani kwa

kiwango kikubwa husawiri hali za jamii husika. Hii ndiyo sababu inayochangia kuwepo kwa tofauti katika fasihi kutoka jamii moja hadi nyingine.

Suala la mtunzi wa kazi ya fasihi kuzingatia upekee wa lugha anaporejelea miktadha mbalimbali ya kijamii lina uamilifu wa kuipa uhalisia kazi husika. Uchunguzi wetu unajikita hasa katika mchango wa sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Uchunguzi huu umechangiwa na msukumo kuwa kuna vigezo mbalimbali vya kijamii ambavyo huathiri mitindo ya matumizi ya lugha katika jamii. Baadhi ya vigezo hivi ni pamoja na lengo la mzungumzaji, kazi wanazofanya, umri wa wahusika katika mazungumzo, mada inayotawala katika mazungumzo na kadhalika.

Azimio la uchunguzi wetu linatokana na ukweli kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya lugha na jamii. Fasihi imewahi kuelezwa kama kioo cha jamii kwa madai kuwa huangazia mambo ambayo yanajiri katika jamii mahususi. Ni hali hii ambayo huzua tofauti katika fasihi ya jamii moja na nyingine. Kwa mfano, methali za watu wa pwani huafiki shughuli za huko kama vile uvuvi. Hata hivyo, tunatambua kuwa fasihi si kioo cha jamii tu lakini inakiuka mipaka hiyo na kuwa na utendakazi mwingine. Kutokana na hali hii, tulipata msukumo wa kuchunguza jinsi msanii wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* alivyodhihirisha muktadha halisi wa dini ya Kikristo katika kazi zake.

1.4 Maswali ya utafiti

Utafiti wetu utaongozwa na maswali yafuatayo:

- i. Je, ni sifa gani zinazofungamana na sajili ya dini ya Kikristo zilizoangaziwa na mwandishi?
- ii. Je, ni michakato ipi ambayo huwawezesha wafuasi wa dini ya Kikristo kufasiri semi zinazohusiana na dini ya Kikristo?
- iii. Je, matumizi ya sajili ya dini ya Kikristo yana mchango gani katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*?

1.3 Madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti wetu ni pamoja na:

- i. Kufafanua sifa za sajili ya dini ya Kikristo zinavyojitokeza katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*.
- ii. Kuonyesha michakato ambayo wafuasi wa dini ya Kikristo na wasomaji wa *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* wanatumia kufasiri semi zinazofungamana na sajili ya dini ya Kikristo.
- iii. Kudhihirisha mchango wa matumizi ya sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*.

1.5 Sababu za kuchagua mada hii

Lugha ni nyenzo kuu ya kuwawezesha binadamu kuwasiliana. Hivi ni kusema kuwa lugha ni nguzo kuu inayomwezesha binadamu kuendeleza harakati muhimu katika jamii kama vile imani za kidini. Uchanganuzi wa sajili katika kazi tulizotaja ni muhimu kwani

utawapa watunzi wa kazi za fasihi ari kuzingatia suala la upekee wa matumizi ya lugha katika kazi zao wanapozungumzia masuala mbalimbali ya kijamii. Katika dini, lugha ina jukumu la kuonya, kukaripia, kuelimisha na kadhalika. Lugha ya dini hasa ya Kikristo hujulikana kusheheni vitisho, ushawishi na msamiati maalum.

Kuna uchunguzi uliowahi kufanywa kuhusu mtindo wa lugha katika ujumla wake na mtindo kama sajili na wataalam kama vile Crystal (1997). Iribemwangi na Mukhwana (2011) wakimrejelea Crystal (1997) wanaieleza sajili kama aina ya lugha inayoelezwa kutegemea matumizi yake katika hali tofauti tofauti za kijamii. Katika uchunguzi wetu tuliangazia sajili ya dini ya Kikristo kama ilivyodhihirishwa na Ken Walibora katika riwaya zake: *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Aidha, tunadhamiria kuangazia mchango wa sajili hii katika kumwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Utafiti wa sajili kama inavyojitokeza na kutumika katika matini haujatafitiwa sana. Hali hii inatupa ujasiri wa kusema kuwa utafiti wetu utakuwa wenye manufaa.

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Suala la lugha ni pana sana na haiwezekani kuyashughulikia masuala yote katika lugha kwa wakati mmoja. Tumeshughulikia sajili ya dini ya Kikristo kama inavyobainika katika kazi za Ken Walibora: *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Kauli hii ina maana kuwa tulishughulikia sajili hii kimaandishi tukijikita katika nadharia ya pragmatiki leksika.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii

Kwa mujibu wa Crystal (1969) mzungumzaji hawezi kutumia mtindo mmoja wa mazungumzo akizungumza na makundi tofauti ya watu. Anazidi kusema kuwa mzungumzaji hana budi kuelewa mahitaji ya hadhira yake anapotumia lugha. Katika maelezo yake anazungumzia vipengele vitatu ambavyo aliviona muhimu kuzingatiwa na wazungumzaji: aina ya hadhira, mahitaji ya hadhira na mada inayozungumziwa. Kwa mujibu wa haya madai ya Crystal ni bayana kuwa waandishi wa kazi za kisanaa hawana budi kutumia mitindo tofauti ya lugha wanapoangazia masuala na miktadha mbalimbali ya kijamii katika kazi zao.

Lugha ya dini ya Kikristo haina budi kutofautiana na lugha inayotumiwa katika miktadha mingine ya kijamii. Hii inatokana na ukweli kuwa lugha hii hujikita katika mada mahususi. Kean (1997) anadhihirisha kuwa lugha ya kidini inatofautiana na mazungumzo ya kila siku. Kutokana na maelezo ya Kean, ni bayana kuwa lugha ya dini kwa jumla ina sifa zake bainifu. Baadhi ya sifa hizi za kijumla za lugha ya dini ni kama vile kutaja majina ya vitabu vitakatifu, kutaja majina ya Mungu au miungu husika, lugha inayodhihirisha unyenyekevu na kadhalika. Hali hii inatokana na ukweli kwamba lugha ya kidini kwa kiwango fulani hujikita kwenye mada mahususi.

King'ei (1992) anasema kuwa mtindo wa lugha ya kidini huwa tofauti sana na matumizi ya lugha ya kawaida. Anaendelea kusema kwamba ni vigumu kufahamika na watu wasioitumia lugha hii na muktadha wake wa matumizi. Anadokeza kuwa mtindo wa lugha ya kidini huwa tofauti sana na matumizi ya lugha ya kawaida. Aghalabu watu

wasiotumia lugha hii ya kidini na muktadha wake hukosa kuufahamu. Uchunguzi huu ni muhimu kwetu kwani ulituwezesha kutambua kuwa lugha ya dini kwa jumla ni ya kipekee. Kazi hii ni tofauti na yetu kwani tunadhamiria kuchunguza jinsi mwandishi wa *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* alivyotumia lugha ya kipekee anaporejelea masuala ya dini ya Kikristo.

Mutiso (1996) alilishughulikia umbo asili la motifu katika shairi la *Kasida ya Burudai* ambalo linajadili masuala ya dini ya Kiislamu. Alishughulikia ishara na uashiraji mbalimbali unaopatikana katika shairi hilo katika dini ya Kiislamu. Uchunguzi wetu ni tofauti na huu kwani unahusu sajili ya dini ya Kikristo kimaandishi katika riwaya teule.

Mathooko (2007) anasema kuwa kuna uwezekano wa matumizi ya lugha ya kigeni katika sajili ya kidini. Mfano mzuri ni lugha za Kilatini na Kiyunani zinazotumika katika vitabu vya dini ya Kikristo. Sajili ya dini ya Kikristo hudokeza maneno yanayotaja Mungu ambayo huanza kwa herufi kubwa. Kazi hii ilitufaa sana katika uchunguzi wetu kwani ilituwezesha kubaini sifa za lugha ya dini ya Kikristo. Madai haya ya Mutiso ya kuwepo kwa matumizi ya misamiati ya kigeni kama vile kutoka lugha za Kiyunani yana mashiko. Katika sajili ya dini ya Kikristo, kwa mfano, kuna maneno yenye asili ya kigeni kama vile halleluyah, Yahweh, Jireh, hosanna Elshadai, Elohim na kadhalika.

Indede (2007) alishughulikia lugha ya kitamaduni katika mahubiri ya dini ya Kikristo kwa kujikita katika sitiari na tashbiha akiongozwa na nadharia ya umaanisho ya Grice. Katika uchunguzi wake alibainisha baadhi ya sitiari na tashbiha ambazo hutumika katika

mahubiri ya dini ya Kikristo. Kazi yetu kwa kiwango fulani ni tofauti na yake kwani sisi tulidhamiria kudhihirisha mwandishi wa kazi teule alivyotumia lugha ya kipekee katika kurejelea masuala ya dini ya Kikristo katika matini teule. Ni dhahiri kuwa lugha ya dini ya Kikristo husheheni tashbihi na sitiari hali ambayo huzua taswira zinazokusudiwa na wazungumzaji husika. Uhusiano uliopo kati ya uchunguzi wetu na wake ni kuwa sisi tunachunguza sifa za lugha ya dini ya Kikristo ambapo baadhi yazo ni tashbihi na sitiari. Tulidhamiria kudhihirisha namna mwandishi wa *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* alivyotumia lugha ya kipekee katika kurejelea masuala ya dini ya Kikristo katika kazi zake.

Bitinyu (2011) katika tasnifu yake anaeleza kuwa dini ni sehemu moja ya utamaduni wa watu lakini dini ambazo zinakuja zina ubepari mwingi. Kazi hii ina uhusiano na uchunguzi wetu kwa vile inaangazia suala la dini linalopatikana katika riwaya za *Utengano* na *Paradiso*. Tofauti iliyoko kati ya kazi yetu na yake ni kuwa wakati ambapo anaichunguza dini katika mtazamo wa kimaudhui nasi tulichunguza katika mtazamo wa sajili katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*.

Uchunguzi wa Bitinyu unaoana na wetu kwa kiwango fulani kwa vile sifa za dini zinazojitokeza katika kazi alizoshughulikia ndizo zilimwezesha kutambua maudhui ya dini. Hii ni kwa sababu lugha ya kidini hutambulishwa na sifa mahususi. Katika kazi yetu, tuliangazia suala la kufasiri semi za dini ya Kikristo mbali na kuonyesha nafasi ya lugha ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*.

Okombo (2011) alifanya uhakiki wa kimtindo wa sitiari, taashira na tashbihi katika utenzi wa *Tambuka*. Alishughulikia dhana na aina za tamathali za usemi pamoja na uamilifu wake. Licha ya kuwa uchunguzi wake ulihusu lugha ya dini, ni tofauti kwa kiwango fulani na wetu unaojikita katika dini ya Kikristo. Hata hivyo, kazi hii ilitufaa katika utafiti wetu kwani kuna uwiano fulani katika sifa za lugha ya dini ya Kiislamu na ya Kikristo.

Nthenya (2012) aliangazia mikakati ya mawasiliano wanaotumia wakalimani kwa kulenga makanisa ya Kipentekoste katika makanisa teule katika mji wa Machakos nchini Kenya. Uchunguzi huu unahusiana na wetu kwa kuwa unajikita katika sajili ya dini ya Kikristo sawa na sisi. Mpaka uliopo kati ya kazi na yetu ni kuwa yeye anachunguza sajili ya dini kiusemi nasi tunaichunguza kimaandishi. Kazi hii ilitufaa kwa vile itatuwezesha kubaini sifa za sajili ya dini ya Kikristo.

Waweru (2012) alichanganua ubadilishaji wa msimbo katika kanisa Katoliki akiongozwa na nadharia ya umaanisho ya Grice (1975). Kutokana na usomaji wa kazi yake ni bayana kuwa alishughulikia uhusiano wa lugha na dini kwa jumla. Uchunguzi huu ulitufaa katika kubainisha sifa za sajili ya dini ya Kikristo kwani ulihusu dini.

Rahim (2012) anadhihirisha namna mwingiliano kati ya lugha na dini ulivyopuuzwa na wanaisimu nchini Iran ilhali vitengo hivi viwili vina uhusiano muhimu miongoni mwa watu. Anaendelea kusema kuwa mazungumzo ya kawaida hayahitaji lugha maalum kama ya dini yanavyohitaji kwani muktadha wa kidini na mazingira yake yanahitaji maneno maalum. Utafiti huu ulitufaa kwa kutuwezesha kutambua na kuchanganua sifa za sajili ya

dini ya Kikristo kama ilivyojitokeza katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*.

1.8 Msingi wa kinadharia

Katika uchunguzi wetu tuliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika. Nadharia hii iliasisiwa na Blutner katika mwaka wa 1990. Katika nadharia hii alionyesha jinsi maana ya neno kiisimu ilibadilishwa katika matumizi. Yaani maana ya neno hufasiriwa kulingana na muktadha fulani wa matumizi. Pragmatiki leksika inachunguza jinsi wazo lililowasilishwa kwa kutumia neno lilitofautiana na dhana iliyosimbwa kisemantiki.

Blutner (2011) anasema kuwa nadharia ya pragmatiki leksika ilianzishwa na McCawley mnamo mwaka wa (1978) akirejelea nadharia ya Grice, (1967) ya mazungumzo. Katika nadharia hii alionyesha kuwa tofauti kati ya muundo wa isimu na maana iliyosimbwa na fasiri iliyopendekezwa ni matokeo ya kanuni za kijumla za ushirikiano na huenda hatua kwa hatua zilizotabirika. Blutner anasema kuwa nadharia ya pragmatiki leksika inachunguza michakato ambapo maana mahususi ya neno hubadilika kutegemea matumizi katika muktadha. Yaani maneno huchanganuliwa kwa utaratibu na kufasiriwa kutegemea muktadha wa matumizi.

Tunaweza kueleza pragmatiki kama somo linalohusu maana kimuktadha. Hii ina maana ya ufasiri wa kile watu wanamaanisha katika muktadha mahususi na jinsi muktadha huathiri ufasiri wa kinachosemwa. Huangazia kile kinachomaanishwa bali si kilivyosemwa. Hii ina maana ya kwamba mengi yanayosemwa hutambuliwa kama

kiungo cha yaliyosemwa. Grice (1989) anapendekeza kuwa kuna mseto unaoonekana wa chukulizi zinazoelekeza jinsi ya kufanya maongezi. Kwa mujibu wa Yule (1996) akizungumzia kanuni ya ushirikiano katika mawasiliano maneno yaliyosemwa yana jumbe nyingi zaidi kuliko yalivyosemwa kwa maana kuwa maneno yanaweza kufasiriwa yakawa na maana nyingi.

Kwa jumla tunaweza kusema kuwa pragmatiki ni somo linalotalii maana ya msemaji au mzungumzaji. Pragmatiki hujishughulisha na maana inavyowasilishwa na mzungumzaji au mwandishi na kufasiriwa mpaka kwa msikilizaji au msomaji. Aidha, huchunguza maana kimuktadha. Yaani ufasiri wa kile watu wanakimaanisha katika muktadha mahususi na jinsi muktadha huathiri maana ya kinachosemwa. Ujumbe mwingi huwasilishwa kuliko ule unaosemwa. Somo hili huangazia vile mengi ya yasiyosemwa hutambuliwa kama kiungo cha yaliyowasilishwa.

Wakati usemi fulani unatolewa na mzungumzaji, msikilizaji hukabiliwa na jukumu la kubaini maana inayokusudiwa. Msikilizaji huenda asipate maana mwafaka ya usemi fulani endapo hatatumia mchakato mwafaka kutambua ujumbe aliokusudia kuwasilisha msemaji.

Blutner (2011) akimrejelea Wilson (2003) na Carston, (2002) anasema kuwa lengo la pragmatiki leksika ni kueleza michakato inayotumiwa katika ufasiri wa maana iliyosimbwa katika usemi na kutatua ugumu wa mawasiliano. Michakato hii ndiyo

hutofautisha dhana iliyowasilishwa na iliyosimbwa katika semantiki. Michakato aliyoangazia kimsingi inayoshughulikiwa katika pragmatiki leksika ni pamoja na kubanika kwa neno, kupanuka kwa neno na kukisia kwa neno.

1.8.1 Kubanika kwa neno

Dhana ya kubanika kwa neno ilitumika kurejelea hali ambapo maana ya neno huwa finyu kuliko maana iliyosimbwa kisemantiki. Hata hivyo, ilidaiwa kuwa hiyo maana finyu ni sharti iwe na uhusiano na muktadha husika. Wilson na Cartson (2007) walitoa mfano wa neno *kunywa* ambalo kwa kawaida huwa na maana ya kutia kitu kiowevu kinywani na kukimeza. Hata hivyo, alisema kuwa neno hili limewahi kufasiriwa kwa maana ya kulewa. Alieleza kuwa hali ya muktadha hufungia nje maana nyingine yote na kuruhusu ufasiri mmoja wa neno lililotajwa kama kubanika kwa neno.

Kutokana na maelezo haya tunaweza kusema kuwa ufasiri wa neno au dhana yoyote ile hutegemea kwa kiasi kikubwa muktadha wa matumizi. Isitoshe, kuna vigezo vingine ambavyo huamua namna ya kufasiri semi mbalimbali zinazotolewa na mzungumzaji. Kwa mfano, mtu akiwa na mwegemeo fulani wa kidini huenda akawa na mazoea ya kutumia semi zinazohusiana na dini husika hata anapokuwa nje ya muktadha wa dini husika. Kwa sababu hii watu anaoingiliana nao hulazimika kufasiri usemi wake kwa kuzingatia mwegemeo wake wa kidini. Viongozi wa kidini kwa mfano aghalabu huwa na mazoea ya kutumia semi zinazoambatana na dini zao hata wanapokuwa nje ya muktadha wa kuabudu.

Kuna mifano anuai ya semi ambazo zinapotumika ama katika muktadha wa dini ya Kikristo au na wafuasi wa dini ya Kikristo huwalazimisha wasikilizaji kuzibana kimaana ili kupata fasiri zake. Mfano wa semi hizi ni neno “bwana” ambalo linapotumika katika muktadha wa dini ya Kikristo hufasiriwa kwa maana ya “Yesu” Hii ina maana kuwa neno hili hubanwa kimaana kutokana na ukweli kuwa lina maaana kadha wa kadha. Neno hili linaweza kutumiwa kumaanisha mwajiri wa mtu, mume wa mtu, tajiri au kihisishi. Hata hivyo, linapotumiwa katika muktadha wa dini ya Kikristo maana nyingine yote hufinywa ili maana moja pekee itiliwe maanani.

Kuna pia semi nyinginezo ambazo zinapotumiwa katika muktadha mingineyo hubanwa kimaana. Kwa mfano neno “chai” lina maana zaidi ya moja. Neno hili linaweza kutumika kumaanisha rushwa au hongo, majani ya chai au kinywaji kinachotengenezwa kwa kutumia majani ya chai. Mtu anapoingia hotelini na kuomba aletewe chai, wahudumu wa hotelini hufungia nje maana nyingine za neno hili na kuchukua maana moja pekee ambayo ni aina ya kinywaji.

1.8.2 Kupanuka kwa neno

Dhana ya kupanuka kwa neno ilitumiwa kurejelea hali ambapo neno lenye maana finyu hutumika kutoa maana ya kijumla. Yaani maana ya neno hupanuliwa kuliko ilivyo kwa kawaida. Blutner (2011) akimrejelea Sweetser (1990) anatoa mfano wa neno *ona* ambalo maana yake ya kisemantiki ni kutazama. Anasema kuwa maana ya neno hili inaweza kupanuliwa hadi likawa na maana ya kuwa na picha ya kitu fulani akilini. Neno hili lenye

maana finyu ya kutazama linaweza kutumika kutoa maana nyingine kimuktadha kuhusu picha.

Lugha ya dini ya Kikristo ina baadhi ya istilahi zenye maana fulani kisemantiki ambazo huishia kupanuliwa kimaana na kuwa na maana ya jumla. Kwa mfano, neno “kesha” lina maana ya kisemantiki ya kukaa macho usiku kucha bila ya kulala. Neno hili aghalabu hupanuliwa kimaana linapotumika katika muktadha wa dini ya Kikristo ili kuleta maana kuomba usiku kucha. Maana hii inadhihirisha kupanuka kimaana kwa vile ile maana yake kisemantiki haileti dhana ya kuomba bali kukaa usiku kucha bila ya kulala.

Neno jingine ambalo limetumika kwa njia hii ni “shiba”. Neno hili hupanuliwa kimaana katika jamii ya Wanyore (Magharibi mwa Kenya) hasa linapotumiwa na walevi. Kisemantiki neno hili lina maana ya kutosheka na chakula baada ya kula au kutokuwa na nafasi tumboni baada ya chakula kujaa. Hata hivyo, neno hili linapotumika miongoni mwa walevi katika jamii husika hufasiriwa kama kulewa kupindukia. Kwa hivyo, mtu anapoonekana akiyumbayumba kwa sababu ya ulevi watu hutoa kauli kama vile, “Huyo ameshiba” kwa maana ya “Huyo yuko chakari”. Aidha, neno gilasi hupanuliwa kimaana ili kurejelea pombe. Kisemantiki neno hili lina maana ya kitu cha kunywa vitu vioweve lakini katika jamii hii hutumiwa kumaanisha pombe kutokana na ukweli kuwa aghalabu pombe huandaliwa walevi kwa gilasi.

Wamitila (2008) anasema kuwa upanuzi huu wa kimaana hutokea pale ambapo maana ya neno inapanuliwa na kuwa na maana ya jumla. Upanuzi wa kimaana waweza kuchochewa na mazingira ya matumizi ya lugha-yaweza kuwa ya kijamii, kisiasa au kisaikolojia. Anatoa mfano wa neno *kupe* lenye maana finyu ya aina ya mdudu mdogo ambaye huganda kwenye miili ya wanyama na kuwafyonza damu. Anaeleza kuwa neno hili linaweza kuwa na maana ya mtu anayewategemea wengine.

1.8.3 Kukisia kwa neno

Hii ni hali ambapo ufasiri wa neno lenye maana finyu linapanuliwa kimaana ili kuhusiana na maana ya kitu kinachohusiana nacho ambacho kina maana tofauti na maana halisi ya neno hilo kiisimu. Kwa mfano, neno *karatasi* katika jamii ya Wanyore katika Magharibi mwa Kenya limewahi kutumiwa kurejelea ugonjwa wa ukimwi. Hii ni kwa sababu mtu anayeugua ukimwi hukondeana na kuwa mwepesi kama karatasi.

Baadhi ya semi za lugha ya Kikristo huweza kufasiriwa wakati ambapo msikilizaji hulazimika kuzifasiri kwa kuzihusisha na kitu kinachohusiana nacho ambacho kina maana halisi ya semi hizo kiisimu. Watu wengine huenda wakarejelewa kwa kutumia majina yanayopatikana kwenye Biblia yanayotaja watu waliokuwa na sifa sawa na zao. Kwa mfano, watu ambao huwa na ugumu wa kusadiki mambo hasa yanayohusiana na imani za kidini hubandikwa jina Tomasi licha ya kuwa na majina yao halisi. Hii ni kutokana na kisa cha Biblia ambapo mtu aliyetitwa Tomasi alidhihirisha kutoamini kwake kuwa Yesu alikuwa amefufuka hadi alipojionea kwa macho yake mwenyewe.

Usemi mwingine ambao hufasiriwa kwa kukisia maana katika muktadha wa kidini ni kama vile “kuvuna”. Usemi huu unapotumiwa ama na wafuasi wa dini ya Kikristo au katika muktadha wa dini ya Kikristo humaanisha kuwafanya watu washawishike kufuata imani ya dini ya Kikristo. Hali ya kuwashawishi watu kuwa wafuasi wa dini inalinganishwa na kuvuna kwa vile wanaohusika huzunguka huku na kule wakitafuta watu ambao watawashawishi waokoke. Aidha, wao hukumbana na changamoto wanapokuwa katika shughuli hiyo jinsi wale wavunaji wa kawaida hukumbana na hali ngumu wanapovuna kama vile hali mbaya ya anga.

Nadharia ya pragmatiki leksika ilitufaa katika utafiti wetu kwani ilitufaa kufasiri semi za sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Dhana za kupanuka kwa neno, kukisia kwa neno na kubanika kwa neno zilitufaa katika kutofautisha maana ya kileksika katika matini na maana ya kimatumizi. Lugha ya dini ya Kikristo husheheni istilahi nyingi ambazo huwahitaji wafuasi wa dini husika kuzifasiri kimatumizi bali si kiisimu.

Dhana ya kupanuka kwa neno ilitufaa katika kufasiri semi mbalimbali zinazofungamana na dini ya Kikristo ambazo humlazimu msikilizaji kuziongezea maana ili kubaini maana inayokusudiwa. Zaidi ya hayo, kuna semi ambazo hufasiriwa kwa urahisi kwa kuzibana kimaana. Hii ni kwa sababu semi hizi zina maana zaidi ya moja. Kuna baadhi ya semi zinazotumika katika dini ya Kikristo ambazo maana yake kileksika hupuuzwa na badala yake kufasiriwa kwa kuzihusisha na semi au hali fulani ili kukisia maana.

1.9 Mbinu za utafiti

Uchunguzi wetu ulijikita katika uchanganuzi wa matumizi ya sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* zilizoandikwa na Ken Walibora. Lengo kuu la utafiti wetu lilikuwa kubaini jinsi mwandishi alivyotumia lugha yenye sifa za kipekee anaporejelea masuala ya dini ya Kikristo. Mbali na haya, tulikusudia kudhihirisha jinsi matumizi ya sajili hii yalivyomwezesha mwandishi kuyafikia malengo yake.

Utafiti huu ni wa maktabani. Tulisoma makala mbalimbali ili kuona uchunguzi unaohusiana na kazi yetu uliofanywa hapo awali na wataalam wengine kisha kupitia kazi nyingine zilizofanywa na wahakiki zilizo na uhusiano na mada hii. Katika kuzisoma kazi hizi tulijaribu kubaini uhusiano zilizokuwa nazo na mada yetu pamoja na kubaini pengo lililopo lililohitaji kuzibwa.

Mbali na kuyasoma makala mbalimbali yanayohusiana na mada yetu tulisoma riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*. Baada ya kuzisoma, tulidondoa maneno, vifungu vya maneno, sentensi pamoja na aya kutoka kwenye kazi hizi ili kuiweka wazi lugha inayohusiana na dini ya Kikristo inayojitokeza katika riwaya hizi. Zaidi ya haya, tuliichanganua data hii kwa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika ili kuweza kudhihirisha jinsi hadhira ya riwaya hizi huweza ikafasiri lugha ya dini ya Kikristo.

1.10 Hitimisho

Mada yetu ya utafiti imehusu “Mchango wa Sajili ya Dini ya Kikristo katika Riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*”. Riwaya hizi zimeandikwa na Ken Walibora katika vipindi tofauti. Hata hivyo, amedhihirisha matumizi ya lugha ya kipekee anaporejelea masuala yanayohusiana na dini ya Kikristo katika kazi hizi mbili. Tulikusudia kutambua jinsi jamii inaathiri matumizi ya lugha katika riwaya hizi hasa masuala ya dini ya Kiristo yanapohusika.

Malengo yetu ya utafiti yamekuwa kuonyesha sifa za sajili ya dini ya Kikristo zinavyojitokeza katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*, kuonyesha michakato ambayo huenda ikaiwezesha hadhira ya *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* kufasiri lugha inayohusiana na dini ya Kikristo na kuonyesha mchango wa sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi*. Ufafanuzi wa njia ambazo huwawezesha wafuasi wa dini ya Kikristo pamoja na wasomaji wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* kuifasiri lugha inayohusiana na sajili ya dini ya Kikristo ulijikita kwenye michakato mitatu iliyofafanuliwa na Wilson (2003) na Cartson (2002) katika nadharia ya pragmatiki leksika.

Nadharia ya pragmatiki leksika iliasisiwa na Blutner katika mwaka wa 1990 ambaye aliieleza kama nadharia inayohusu ufasiri wa maana ya semi kimuktadha. Michakato ya kutekeleza ufasiri wa semi mbalimbali kimuktadha aliyozungumzia kama vile na kupanuka kwa neno, kubanika kwa neno na kukisia kwa neno ilituwezesha kuangazia

ufasiri wa lugha ya dini ya Kikristo katika kazi yetu. Aidha, tulionyesha sifa za sajili ya dini ya Kikristo zinazodhihirika katika riwaya hizi kisha kuangazia uamilifu wa sajili ya dini ya Kikristo katika kumwezesha mwandishi kuuwasilisha ujumbe aliokusudia kuuwasilisha.

SURA YA PILI

UDHIHIRIKAJI WA SAJILI YA DINI YA KIKRISTO KATIKA RIWAYA ZA

KIDAGAAA KIMEMWOZEA NA NDOTO YA ALMASI

2.1 Utangulizi

Kila jamii ina utamaduni wake ambao huathiri matumizi ya lugha kwa njia moja au nyingine. Utamaduni huu ndio husababisha kuwepo kwa mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha katika jamii ambayo hujulikana kama sajili. Mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha hudhihirika katika kazi yoyote ile ya fasihi. Hali hii inatokana na ukweli kwamba fasihi yoyote ile huwa zao la utamaduni maalum.

Riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndotu ya Almasi* zimedhihirisha matumizi ya sajili ya dini ya Kikristo. Katika sura hii tumeshughulikia sifa za lugha ya dini ya Kikristo kama zilivyodhihirika katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndotu ya Almasi*. Kwa kawaida kila sajili ina sifa zake maalum ambazo huitambulisha na kwa kiwango fulani huitofautisha na sajili nyingine.

Mwandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndotu ya Almasi* amedhihirisha lugha ya kipekee kila anapozungumzia masuala yanayohusiana na dini ya Kikristo. Riwaya zote mbili zinaangazia masuala anuai ya kijamii kama vile ukoloni mamboleo, siasa, dini, dhuluma na unyanyasaji wa wanyonge. Ili kuliangazia suala la kidini kwa njia wazi, mwandishi amemakinika katika uteuzi wa lugha anayotumia.

2.2 Msamiati wa kipekee

Ipara na Maina (2008) wanasema kuwa lugha ya kidini ni ya kipekee kwani huwa na maneno mengi ya kumsifu Mungu. Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* mwandishi ametumia msamiati maalum katika kuyarejelea masuala ya dini ya Kikristo. Msamiati huu unaweza kuainishwa katika makundi mbalimbali:

2.2.1 Msamiati unaotaja Mungu na Yesu

Mathooko (2007) anasema kuwa kuna uwezekano wa matumizi ya lugha ya kigeni katika sajili ya kidini. Kwa mfano, kuna lugha za Kilatini na Kiyunani zinazotumika katika vitabu vya dini ya Kikristo. Sajili ya dini ya Kikristo hudokeza maneno yanayotaja Mungu ambayo huanza kwa herufi kubwa. Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* Mama anasema, “Hebu nisubiri niingie chumbani nishauriane na Mungu” (uk114).

Katika muktadha huu Mama alikuwa amesema ameitwa kwenda mbinguni kwa Baba kwa vile alikuwa ameikamilisha kazi yake duniani. Anasema maneno haya baada ya muda aliokuwa amedai kuwa angepaa mbinguni kuisha bila yeye kupaa alivyokuwa amedai hapo awali. Neno “Mungu” limetumika kumaanisha mwenye kuumba mbingu na vyote vilivyomo ndani yake. Katika riwaya ii hii ya *Ndoto ya Almasi* mhusika anayejulikana kwa jina Masasi anasema mambo yafuatayo:

Yeso Kristo yaani aliubiri kwa mulima miaka silisopita yaani na mimi nafuata nyayo sake kwa kuubiri kutoka chuu ya ...ili yaaani nyinyi watu wa Cherengani musikie. Sasa maandiko nasema kama macho yako mocha yaani nafanya wewe nafanya tambi, ng’oa. Yaani ona pila macho hio kapisa. (uk.147)

Majina “Yeso Kristo” yametumiwa kurejelea kiumbe cha kimbinguni ambacho kinaaminiwa na wakristo kuwa ni mwana wa Mungu na kwamba aliwahi kuishi humu duniani kabla ya kufa na kufufuka kisha kurudi mbinguni. Kuna matumizi ya neno “malaika” lililotumiwa kurejelea kiumbe wa kimbinguni wa kiroho anayebainishwa na umbo la kibinadamu mwenye mbawa. Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* mama anasema, “Mimi kile najua kwamba huko juu mbinguni shangwe ni tele kwa malaika mwenye dhambi mmoja anapotubu” (uk.147). Katika kauli hii ya mama Almasi anatumia neno “malaika” ambalo linarajelea kiumbe cha kiroho cha kimbinguni chenye mbawa. Kiumbe hiki huaminiwa kuwa na umbo la binadamu na wanadai kwamba kuna wafuasi wa dini ya Kikristo wanaodai kuwa wamewahi kukiona.

2.2.2 Msamiati unaotaja majina ya watu yanayopatikana katika Biblia

Lugha iliyotumiwa katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* kurejelea masuala ya kidini kwa kiwango kikubwa inahusu kutaja kwa majina ya watu yanayopatikana katika Biblia. Hali hii imetumika ili kuyafanya mazungumzo yenyewe yawe na uhalisia wa dini ya Kikristo katika riwaya hizi. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* mwandishi anasema kuwa Mtemi alichukua Biblia. Anasema, “Safari hii alisoma habari ya Amnoni mwanawe Daudi, kumbaka dadake mwenyewe katika kitabu cha 2 Samueli” (uk.103). Katika usemi huu kuna majina ya watu yaliyotajwa katika Biblia ambayo ni pamoja na Amnoni na Daudi.

Naye mkewe Mtemi Nasaba Bora, Bi. Zuhura anapomwambia mtemi kuwa anafaa kuwaachilia wale vijana alioagiza watiwe ndani ya seli bila hatia, “...kumbe

wanaitwaje vile?”(uk. 104). Naye Bi. Zuhura-mkewe anamjibu, “Amani na Imani” (uk.104). Licha ya kuwa Mtemi Nasaba Bora amelisikia jibu la mkewe, anayageuza maneno yake na kusema: “Ahaa. Amnoni na Tamari” (uk.104).

Mtemi Nasaba Bora anayatumia majina haya ya watu yanayopatikana katika Biblia kimaksudu kuwarejelea wahusika katika riwaya hii ambao ni Amani na Imani kwa vile anadhani kuwa wanashiriki mapenzi. Kwa maoni yake, jinsi hadithi ianaelezwa katika Biblia ambapo mtu aliyeitwa Amnoni alishiriki ngono na dadake halisi aliyeitwa Tamara ndivyo Amani na Imani (anaowajua kama ndugu wa kuzaliwa) walivyohusiana kimapenzi.

Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* Masasi anasema, “Unakumbuka yaani sauti ilitoka mbinguni Yesu alipofika katika mutoni Yortani, ehe, ‘Wewe ni mwanangu mpentwa: nimekukubali wewe’” (uk.38). Masasi anayasema maneno haya baada ya kutangaza wazi kuwa amekuwa mlokole na kwamba ameacha ulevi. Katika usemi huu kuna jina “Yesu” linalopatikana katika Biblia ambalo linarejelea kiumbe cha Mungu kinachoaminiwa na wakristo kuwa ni mwokozi wao.

Katika *Ndoto ya Almasi* kuna mhusika ambaye anatoa kauli yenye majina ya watu yanayopatikana katika Biblia. Anasema, “Kama vile Rebeka alivyoolewa na Isaka na kumpa faraja baada ya kifo cha Sara, mamake” (uk.113). Chebosio anatumia maneno haya anapajaribu kumshawishi Almasi anwoe baada ya kifo cha mamake. Katika usemi

huu kuna maneno yanayotaja majina ya watu yanayopatikana katika Biblia ambao ni “Rebeka” na “Sara”

2.2.3 Msamiati uliosheheni sifa kwa Mungu

Wahusika ambao wamesawiriwa kama wafuasi wa dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* wanatumia lugha iliyosheheni msamiati wenye kusifu Mungu. Hali hii inamwezesha msomaji kuwatofautisha na wahusika walokole wengine. Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* Mama ni mhusika aliyesawiriwa na mwandishi kama mlokole. Hali kama hii inajitokeza anapokutana na wanawe waliokuwa wameitika wito wake wa kuja kushuhudia mama akienda kwa Baba. Katika salamu zake anasema: “Bwana asifiwe” (uk.109). Hii ni kaida ya kuamkuana miongoni mwa wafuasi wa dini ya Kikristo.

2.3 Lugha yenye matumaini

Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* wahusika ambao ni wafuasi wa dini ya Kikristo wanadhihirisha matumizi ya lugha yenye matumaini katika maongezi yao. Almasi anapofika nyumbani anasikia sauti ya mamake aliyokuwa ameikosa kwa muda mrefu akiimba wimbo wake aupendao:

Sendi no musale

Muno mwiloba

Musale wange ni Yesu

Ali mwikulu. (uk.108)

Mimi sina rafiki
Humu duniani
Rafiki yangu ni Yesu
Aliye mbinguni (T.Y)

Tafsiri ya wimbo huu ni kuwa mama anasema kuwa yeye hana rafiki humu duniani bali rafiki yake ni Yesu aliye juu mbinguni. Wimbo huu unadhihirisha matumaini kwani Mama anakumbwa na mateso anuai kama vile ulevi wa mumewe. Hata hivyo ana matumaini kuwa wakati mmoja atafika mbinguni na kukutana na rafiki yake ambaye ni Yesu.

Aidha, katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kuna wahusika waliosawiriwa na mwandishi kama wafuasi wa dini ya Kikristo kama vile babake Mtemi Nasaba Bora. Wahusika hawa wanadhihirisha matumaini katika mazungumzo yao. Mtemi Nasaba Bora anakumbuka siku za utotoni na kuusikia mwangwi wa sauti ya hayati babake aliyekuwa kasisi akiwasomea maandiko:

Petro akafungua kinywa chake akasema: Hakika nawaambia kuwa Mungu hana mapendeleo bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye.
(uk.99)

Usemi huu unadhihirisha matumaini kwa Mungu ya kwamba kila mtu anaweza kukubalika na Mungu mradi anatenda haki na kumcha yeye.

2.4 Kudondoa kauli kutoka katika Biblia

Ipara na Maina (2008) wanasema kuwa ni kawaida katika lugha ya kidini kudondoa kauli yaani mzungumzaji anarejelea sehemu fulani katika maandiko matakatifu. Maandiko matakatifu yaliyonukuliwa katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* ni Biblia. Mwandishi amewasawiri wahusika mbalimbali hivi kwamba wanajitokeza kama wafuasi wa dini ya Kikristo. Aghalabu, wahusika wenye kusawiriwa kama wafuasi wa dini ya Kikristo wananukuu vifungu kutoka kwenye Biblia katika usemi wao. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* Amani anasema, “Nataka ukumbuke tu kwamba hali yangu karibu sawa na ile ya Yusufu na mke wa Potifa” (uk. 147).

Kifungu hiki kinanukuliwa kutoka kwenye Biblia katika kitabu cha Mwanzo ambapo Amani analinganisha hali ya Bi. Zuhura kumtaka wafanye mapenzi na ile hadithi katika Biblia ambapo mke wa Potifa alitaka wafanye mapenzi na Yusufu. Kisa cha Bi. Zuhura kumtaka Amani mapenzi kina uhusiano na kile cha Potifa na Yusufu kwa vile Potifa alikuwa mke wa kiongozi (Farao) naye Bi. Zuhura ni mke wa mtemi wa eneo la Sokomoko.

Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* wahusika waliosawiriwa kama wafuasi wa dini ya Kikristo wanavinukuu vifungu vya Biblia katika usemi wao. Mtemi Nasaba Bora ni mhusika duara. Hii ina maana kuwa anabadilika kitabia. Mwanzoni anadhihirika kama mhusika mwovu mwenye kukufuru dini. Baadaye anabadilika na kuwa mdini mambo yanapomwendea kombo. Katika dayalojia yake na Amani anasema, “Katika maisha

yangu nilidhamiria kutenda mema, nikashindwa. Jema n'takalo kulitenda silitendi; baya nisilotaka kutenda ndilo n'tendalo” (uk.150).

Usemi huu umenukuliwa kutoka kwenye Biblia kama ulivyotamkwa na mtume Paulo katika nyaraka zake. Usemi huu unapotumiwa na Mtemi Nasaba Bora ni ishara kuwa anajutia matendo yake maovu kama vile unyanyasaji, ukatili na ubinafsi.

2.5 Lugha iliyosheheni sifo

Aghalabu lugha ya dini ya Kikristo husheheni matumizi ya lugha yenye kusifu Mungu. Wafuasi wa dini ya Kikristo huamini kuwa wanafaa kummiminia Mungu sifa kwani anastahili sifa. Wahusika waliochorwa kama wafuasi wa dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* wanaonekana kutumia lugha inayodhihirisha sifa kwa Mungu wao. Katika *Ndoto ya Almasi* Mama anapokutana na wanawe anawaamkua salamu kwa kutumia maneno yenye sifa, “Bwana asifiwe” (uk.109).

Almasi anapowasili nyumbani anamkuta Mama akiwa huko ambaye anamwamkua kwa usemi ufuatao, “Ohoo! Bwana asifiwe mwanangu” (uk.151). Bwana anayerejelewa katika usemi huu ni Yesu. Kwa vile Mama ni mhusika aliyesawiriwa na mwandishi kama mllokole anatumia maneno haya ili kuonyesha heshima zake kwa Mungu.

2.6 Lugha yenye unyenyekevu

Aghalabu lugha ya dini ya Kikristo huwa na unyenyekevu kwa vile wafuasi wa dini hii hudhihirisha unyonge wao kwa Mungu ili wapate neema. Wafuasi wa dini ya Kikristo

humwona Mungu kama mwenye uwezo wa hali ya juu ndiposa wao hunyenyekea mbele yake ili waonewe rehema na Mungu.

Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* wahusika wanaojitokeza kama wafuasi wa dini ya Kikristo wanaonekana kunyenyekea au kuhimizana kunyenyekea mbele ya Mungu. Katika *Kidagaa Kimemwozea* tunaelezwa kuwa Nasaba Bora alipomweleza nduguye Majisifu (ambaye siku hizo alikuwa mlokole) kisa chake na yule msichana mlemavu anamwambia kuwa lilikuwa somo kutoka kwa Muumba. Anamhimiza kuwa alipaswa kulikisi tanga lake na kusafisha njia zake ili apate maghufuru ya Mwenyezi Mungu. Usemi huu unaelekea kumshawishi Nasaba Bora kunyenyekea mbele ya Mungu ili asamehewe dhambi zake.

Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* mhusika aliyesawiriwa kama mlokole anatumia lugha yenye unyenyekevu anapomrejelea Mungu. Licha ya changamoto alizokumbana nazo katika ndoa anazidi kunyenyekea kwa Mungu. Baada ya mumewe kutoweka nyumbani na kuenda asikojua, Almasi anamdadisi mamake kila mara akitaka kujua alikokwenda babake. Mama anamjibu kwa usemi ufuatao, “Mungu akipenda mume wangu atarudi siku moja” (uk.154). Neno “akipenda” linaonyesha jinsi Mama alivyonyenyekea kwa Mungu na kutotaka kumlazimisha kuyatekeleza mahitaji yake bali kunyenyekea ili mwenyewe amhurumie.

2.7 Matumizi ya tamathali za usemi

Aghalabu lugha dini ya Kikristo huhusisha tamathali za usemi. Ipara na Maina (2008) wanasema kuwa ni rahisi kutambua sajili ya dini kutokana na matumizi maalum ya tamathali za usemi kama vile mafumbo, taswira, jazanda na istiari.

Yesu Kristo alisifika sana kwa matumizi ya istiari katika ufundishaji wake. Kwa mfano, hadithi yake ya mwana mpotevu aliyemwomba babake urithi wake wote, kuhamia nchi ya mbali kisha kuutumia kwa ubadhirifu. Anapofilisika, anarejea nyumbani ambako anapokelewa na babake kwa sherehe. Istiari hii inakusudiwa kumwonyesha mkristo kuwa anaweza kukubalika na Mungu hata baada ya kutenda maovu.

Aidha, anatumia istiari ya mpanzi mmoja aliyepanda mbegu zikaanguka katika maeneo mbalimbali. Kuna zile zilizoanguka maguguni. Ingawa zilimea hazikunawiri kwani zilikuwa katikati ya magugu. Kuna zilizoanguka mwambani kwa hivyo hazikumea kwa vile hazikupata mazingira mwafaka. Kuna zilizoanguka njiani na zikakosa kumea kwani zililiwa na ndege. Hatimaye kuna zile zilizoanguka katika mchanga mzuri zikamea, kunawiri kisha kuzaa matunda. Istiari hii inatumika kuashiria namna watu wa aina mbalimbali hupokea ujumbe kutoka kwa Mungu kwa njia tofautitofauti.

Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* sifa hii ya matumizi ya lugha imedhihirika kila wahusika mbalimbali waliporejelea masuala yanayohusiana na dini ya Kikristo. Baadhi ya tamathali zinazojitokeza katika riwaya hizi ni pamoja na: mafumbo, jazanda na sitiari.

2.7.1 Jazanda

Lugha ya dini ya Kikristo huwa na matumizi ya mafumbo. Yaani lugha ambayo humhitaji mtu kufikiria ili kujua maana inayokusudiwa. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mafumbo ni kauli ambazo huficha maana fulani kwani kuna jambo ambalo limefumbwa ambalo msikilizaji au msomaji anahitajika kufumbua. Kipengele cha lugha yenye jazanda pia kinajitokeza katika Biblia.

Kwa mfano, katika Biblia kuna maneno ambayo hutumiwa kimaufumbo kama vile neno “Simba wa Yuda” kwa maana ya Yesu. Hii inatokana na ukweli kuwa simba ndiye mnyama anayeogopwa sana na wanyama wengine porini. Yesu analinganishwa na samba kutokana na uwezo na mamlaka aliyo nayo.

Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* kuna baadhi ya semi pamoja na maneno yaliyotumiwa ili kuashiria maana ya ndani na wahusika waliosawiriwa kama wafuasi wa dini ya Kikristo. Mama ambaye anadhihirisha mienendo ya ucha Mungu tangu mwanzoni mwa riwaya hadi mwisho anatumia maneno yenye maana fiche anapozungumza. Almasi anapokuwa shuleni tunaambiwa kuwa, “Almasi alikuwa anafuata nasaha ya mamake ya kutembea na Yesu katika uwanja wa shule ya Mtakatifu Yusuifu” (uk.38). Katika usemi huu kirai “kutembea na Yesu” kimetumiwa kijazanda. Kwa kawaida kutembea ni kusonga hatua moja hadi nyingine kwa kutumia miguu. Hata hivyo, maneno haya yametumiwa kumaanisha kumtii au kufuata mafundisho ya Yesu.

Kwa upande mwingine, Mama anapomsihi Almasi afanye kazi ya Mungu, Almasi anamwambia kuwa hawezi kutakata tena ili afanye kazi ya Mungu kwani ameharibika

sana. Mama anamhimiza kwa kumwambia, “Hakuna kuchelewa mno. Damu ya Yesu itakuosha na itakuosha utakate kama theluji” (uk.25). Maana ya kileksika ya neno “osha” ni kusafisha kwa maji. Hata hivyo, Mama analitumia neno hili kwa maana ya kusamehewa dhambi na kutakaswa kama lilivyotumika katika Biblia.

Kuna maneno mengine yaliyotumiwa kwa maana tofauti na ya maana ya kawaida. Kwa mfano, neno “vita” kwa kawaida hutumika kwa maana ya mapambano kati ya watu au wanyama. Mapambano haya aghalabu hufanyika kwa kutumia silaha zinazoonekana. Mama anapodai kuwa amemaliza kazi yake na kwamba yuko tayari kwenda kwa baba anasema kuwa amepiga vita na kwamba sasa kazi yake duniani imekwisha. Katika usemi huu neno “vita” limetumika kufumbika maana ya kuishi maisha yanayoambatana na mapenzi ya Mungu licha ya pingamizi za shetani.

Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kuna usemi unaoambatana na dini ya Kikristo ambao una maana ya ndani. Kwa mfano, Mtemi Nasaba Bora anamtuma mkewe amletee Biblia kisha anaanza kuisoma. Mkewe Bi. Zuhura anapojaribu kunyanyuka hapo anamwambia akae kitako asikilize neno. Mwandishi anasema, “ Bi. Zuhura anapojaribu kunyanyuka kwenda kutazama kuna nini mumewe kamwambia aketi kitako asikilize neno” (uk.102).

Jina “neni” lina maana ya mkusanyiko wa vitamkwa kama vile konsonanti na irabu. Katika usemi wa Mtemi Nasaba Bora neno hili limetumika kwa maana ya maelekezo, ushauri, maonyo, himizo na ahadi za Mungu kwa binadamu kupitia kwa Biblia. Hii ndiyo

sababu katika muktadha wa dini ya Kikristo watu husema kuwa wamekusanyika ili kusikiliza neno.

Hali hii inatokana na ukweli kuwa wafuasi wa dini ya Kikristo wana mazoea ya kuwalinganisha na watu ambao maisha yao yameelezwa katika Biblia wenye sifa zinazowiana na zao. Kwa mfano, mtu ambaye ni msaliti anaweza kulakabiwa, “Yudasi”

2.7.2 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi inayohusu kulinganisha vitu viwili moja kwa moja ili kujenga taswira fulani katika akili ya mzungumzaji. Sajili ya dini ya Kikristo hutumia sitiari ambapo watu au hali mbalimbali hulinganishwa ili kuchora picha maalum. Katika riwaya hizi kuna matumizi ya lugha yenye ulinganisho wa wahusika wanapozungumzia mambo yenye uhusiano na dini ya Kikristo. Katika *Ndoto ya Almasi* kwa mfano, Mama anasema, “Nimepigana vita vyangu na sasa kazi yangu duniani imekwisha” (uk.109).

Katika kauli hii hali ya mtu kuishi maisha ya kumtii Mungu inalinganishwa na vita. Hii inatokana na ukweli kuwa mtu yeyote anayeishi akimcha Mungu hukumbana na changamoto nyingi. Naye hupambana ili asije akawacha kutenda mapenzi ya Mungu. Hii ndiyo sababu hali hii inalinganishwa na vita.

2.8 Lugha yenye heshima

Lugha ya dini ya Kikristo husheheni matumizi ya maneno ya heshima. Wafuasi wa dini hutumia lugha ya heshima wanapomrejelea Mungu ili wapate rehema za Mungu. Katika

riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi* kuna wahusika wanaokuzwa na mwandishi hivi kwamba wanajitokeza kama wafuasi wa dini ya Kikristo. Katika mazungumzo yao, wanadhihirisha heshima hasa wanapomrejelea Mungu. Aidha, baadhi yao wananukuu vifungu kutoka kwenye Biblia ambavyo vina msamiati wa heshima. Katika *Ndoto ya Almasi* kuna usemi ufuatao wa mama unaodhihirisha maneno ya heshima, “Bwana asifiwe sana” (uk.109). Mama anawaamkua wanawe aliowaalika nyumbani ili washuhudie anapokwenda mbinguni kwa kutumia kifungu hiki, “Naenda mbinguni kwa baba” (uk.110). Katika maelezo yake kwa wanawe mama anatumia kifungu hiki kwa maana ya kuenda mbinguni, “Wanangu mimi namshukuru Bwana mwokozi kwa kuwawezesha kuitika wito wangu mara moja” (uk.109). Katika kauli hii mama anadhihirisha heshima kwa Mungu anapomrejelea kama bwana.

Katika mazungumzo haya yote kuna maneno yanayoonyesha kuwa Mama anampa Mungu heshima. Baadhi ya maneno haya ni “baba” na “bwana”. Kwa kawaida, neno “baba” hutumika mtu anapotaka kumrejelea mzazi wake wa kiume kwa heshima. Nalo neno “bwana” hutumika kama jina la heshima wakati mtu anamrejelea mumewe. Kwa mfano, katika Biblia tunaelezwa kuwa kuna mwanamke aliyeitwa Sara alikuwa akimrejelea mumewe kwa heshima kwa kutumia jina hili.

Katika *Kidagaa Kimemwozea* kuna wahusika walionukuu vifungu vya Biblia vinavyodhihirisha heshima kwa Mungu hasa wanapoonyana dhidi ya maovu. Katika siku ya Uhuru, Balози anawapa wakazi wa Sokomoko hotuba dhidi ya kumkashifu mtemi kwa

kunukuu vifungu kutoka kwenye Biblia. Kwa mfano, kuna neno “Mwenyezi” lilitumika kumrejelea Mungu. Anasema:

Anatambulika kwa fadhili na utu wema wake, si katika eneo hili la Sokomoko tu bali katika Tomoko nzima. Kiongozi aliyeteuliwa na mwenyezi Mungu mwenyewe. Yeyote ajaribuye kumpinga anapingana na kudura za Mwenyezi Mungu (uk.68).

Katika usemi huu ni dhahiri kuwa Balози anawahimiza wakazi wa Sokomoko kumheshimu Mungu. Anasema kuwa kwa vile Mtemi ameteuliwa na Mungu basi watu wanafaa kuheshimu jambo hilo na kwamba wasipingane na Mungu kwa kumpinga Mtemi.

2.9 Hitimisho

Sajili ya dini ya Kikristo ni mtindo maalum wa lugha ambao hutumika na wafuasi wa dini ya Kikristo hasa wanapokuwa katika mahali pa kuabudu. Shughuli za kuabudu zinaweza kufanyika katika maeneo mbalimbali kama vile mahali pa kuabudu, uwanjani au chini ya mti. Hata hivyo, kila anayehusika, awe ni mhubiri mwenye uzoefu au muumini wa kawaida hutumia lugha yenye sifa fulani. Watu hawa huenda wakadhihirisha sifa za kipekee katika usemi wao hata wanapokuwa nje ya muktadha wa maabadini. Popote pale mazungumzo yanayooana na dini ya kikristo hutokea ni sharti lugha inayotumiwa idhihirishe sifa za kipekee.

Baadhi ya sifa zinazotambulishwa na dini ya Kikristo ni pamoja na matumizi ya lugha ya kale yenye kudumisha msamiati wa zamani ili kuhifadhi ujumbe kama ulivyotolewa katika maandishi au mawasiliano ya lugha ya asili. Sifa nyingine ni matumizi ya

msamiati wa kipekee, urudiaji na matumizi ya sentensi ndefu. Isitoshe, lugha hii hutambulishwa na hali ya kudondoa kauli kutoka kwenye Biblia ili kutoa ithibati kwa wafuasi wa dini ya Kikristo kuhusu wanayoambiwa. Riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* ni kazi zinazoangazia hali halisi zinazozikumba jamii husika. Katika hali hizi sajili ya dini ya Kikristo ina utendakazi muhimu.

Katika kuangazia masuala haya yote, mwandishi amedhihirisha lugha yenye sifa za kipekee katika kila mojawapo. Suala la dini ni mojawapo ya maudhui yanayojitokeza katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Suala hili limejitokeza kwa wazi kwani mtunzi wa kazi hizi, kupitia kwa wahusika aliowaumba pamoja na maandishi yake mwenyewe amedhihirisha hali halisi ya muktadha wa dini ya Kikristo.

Miongoni mwa sifa za lugha ya dini ya Kikristo zinazojitokeza katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* ni matumizi ya mbinu za lugha kama vile mafumbo, sitiari na taswira. Zaidi ya haya, kuna unukuzi wa kauli kutoka kwenye Biblia, matumizi ya lugha inayotoa sifa na heshima kwa Mungu. Sifa hizi pamoja na sifa nyingine za sajili ya dini ya Kikristo zinazodhihirika katika riwaya zote hizi.

SURA YA TATU

UFASIRI SAJILI YA DINI YA KIKRISTO ILIVYOTUMIKA KATIKA RIWAYA ZA *KIDAGAA KIMEMWOZEA NA NDOTO YA ALMASI*

3.1 Utangulizi

Katika sajili ya dini ya Kikristo kuna semi mbalimbali ambazo hutumika kipragmatiki kwa sababu maalum. Baadhi ya semi hizi hutumiwa ili kuisisimua hisia za wasomaji au wasikilizaji, kueleza hali fulani ambayo ni muhali kueleza kikawaida. Baadhi ya semi hizi hutumiwa ama kwa kukusudia au wakati mwingine bila kukusudia.

Katika sura hii tumeangazia fasiri ya semi zinazotumika katika muktadha wa dini ya Kikristo kama zinavyojitokeza katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Ni bayana kwamba maneno ambayo yamesemwa vizuri na mtu anayefaa kwa wakati unaofaa na taswira kuundwa vizuri yanaweza kuwa na athari kubwa kwa msikilizaji. Kwa mujibu wa Hills (1997), aghalabu muundo wa lugha ya sajili ya dini ya Kikristo hutokana na muktadha na hali.

Mbali na muktadha wa hali kuna mambo mengine ambayo hujenga sajili. Kwa mujibu wa Lawless (1988), makundi na utamaduni hukuza lugha maalum zinazoeleweka tu na wanakikundi hicho. Lugha hii maalum huenda ikachora mipaka na kuwatenga wanakikundi hao na vikundi vya watu wengine katika jamii. Mwongozo wa maneno haya hutokana na Biblia na yana maana maalum kwa watu wanaoyatumia. Maneno mengi katika sajili ya dini ya Kikristo yana maana ya undani hivi kwamba huenda watu wasio wa dini hii wasielewe maana yake.

Hills (1997) anasema kuwa lugha inapata makusudio yake kutokana na muktadha wa jamii. Uchunguzi wetu katika sura hii ulihusu njia ambazo huenda zikaweza hadhira ya riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kufasiri lugha ya sajili ya dini ya Kikristo iliyojitokeza katika kazi hizi.

Uchunguzi wetu umezingatia nadharia ya pragmatiki leksika iliyoasisiwa na Blutner. Blutner (2011) akiwarejelea Wilson (2003) na Cartson (2002) anaeleza mambo ya kimsingi yanayoshughulikiwa katika nadharia ya pragmatiki leksika kama ifuatavyo:

Kupanuka kwa neno

Kubanika kwa neno

Kukisia kwa neno

Hii ni mikakati muhimu katika nadharia hii kwani ndiyo huwawezesha watumiaji lugha kupata fasiri mwafaka ya semi zinazotumika katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Kila mojawapo ya mikakati hii hutekeleza jukumu maalum ambalo humwezesha msikilizaji kupata fasiri mpya ya semi tofauti na ile ya kisemantiki.

3.2 Kupanuka kwa neno

Kupanuka kwa neno ni mkakati wa kufasiri ujumbe ambapo neno linalorejelewa katika hali ya kawaida linatumika kurejelea maana pana zaidi ya maana iliyosimbwa kisemantiki. Kwa kawaida kuna baadhi ya maneno ambayo maana yake hupanuliwa hadi yakawa na maana tofauti na ile iliyosimbwa kisemantiki. Mathalan, neno “jua” lina maana ya kileksika ya kufahamu jambo fulani. Hata hivyo, maana ya neno hili hupanuliwa katika muktadha wa dini ya Kikristo na kutumiwa kumaanisha kufanya

ngono. Hii ina maana kuwa neno hili limeongezea maana mpya katika muktadha wa dini ya Kikristo tofauti na ile ya maana yake ya kisemantiki.

Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kuna semi zilizotumiwa na mwandishi na wahusika mbalimbali ambazo maana yake imepanuliwa hivi kwamba zinaleta maana tofauti na ile iliyosimbwa kisemantiki. Katika sehemu hii, tuliangazia baadhi ya virai na maneno ambayo aghalabu maana yake hupanuliwa hasa yanapotumika katika muktadha wa dini ya Kikristo. Baadhi ya semi hizi ni kama vile:

Vita

Enda

Dada

Nishauriane

Osha

Kutembea na Yesu

Mungu ni mkubwa

Mungu ameniambia

Ng'oa macho

Ona pila macho hio kapisa

Safisha njia

3.2.1 Vita

“Nimepigana vita vyangu na sasa kazi yangu duniani imekwisha” (uk.110). Maneno haya yanasemwa na Mama katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi*. Mama ni mhusika ambaye

amesawiriwa kama mlokole. Maana ya neno vita katika usemi wake imepanuliwa. Hii inatokana na ukweli kuwa maana ya kileksika ya neno hili ni mapambano ya kimwili kati ya watu au wanyama hasa kwa kutumia silaha. Mama ametumia neno hili kipragmatiki kurejela hali ya kuishi kulingana na maagizo ya Mungu. Kwa mujibu wake hivi ni vita kwani inaaminika kuwa mtu yeyote anayefuata maagizo ya Mungu huandamwa na hila za shetani ili amkufuru Mungu. Mama anaiona ile hali ya kung'ang'ana na kuepuka mitego ya shetani kama vita.

3.2.2 Enda

Maana ya neno hili kisemantiki ni hali ya kitu, mtu au mnyama kutoka mahali pamoja hadi mahali pengine. Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* Mama anatumia neno hili kipragmatiki anaposema, “Wakati wangu wa kwenda kwa baba umefika” (uk.110). Katika kauli hii neno kwenda limetumiwa kumaanisha kufa. Kwa watu wengi mtu anapokufa mwili wake hautoweki bali ni uhai unaomwondokea. Wafuasi wa dini ya Kikristo wanaamini kuwa mtu anapokufa roho yake hutoweka na kwenda ama jehanamu au mbinguni kutegemea matendo yake akiwa humu duniani. Hii ndiyo sababu Mama anatumia neno hili si kumaanisha kuwa mwili wake hautatoweka bali kuwa roho yake itaenda mbinguni.

3.2.3 Dada

Neno dada lina maana ya kileksika ya mtu aliye na uhusiano wa kinasaba na mwingine-yaani ndugu wa kike. Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* tunamwona mhusika anayeitwa Magdalina mke wa tatu wa daktari Makabila akilitumia kipragmatiki. Mama anapodai kuwa anataka kwenda mbinguni anamletea barua anayotaka imfikie mwanawe aliyeaga

dunia miaka mingi iliyopita. Anamwambia mamake Almasi yafuatayo, “Dada Paulina tafadhali, tafadhali usiifungue barua hii” (uk.112). Kwa vile Magdalina hajasawiriwa na mwandishi kama mtu aliye na uhusiano wa kinasaba na Paulina, mamake Almasi basi amelitumia neno dada kurejelea mtu yeyoye wa kike mwenye imani sawa ya kidini na yake.

3.2.4 Nishauriane

Maana ya kileksika ya neno kushauri ni ile hali ya kumpa mtu wosia. Mama analitumia neno hili kipragmatiki kuleta maana zaidi ya ile maana ya kisemantiki iliyosimbwa katika neno hili. Hali hii inajitokeza anaposema, “Hebu nisubiri niingie chumbani nishauriane na Mungu kidogo” (uk.114). Mama anumia neno nishauriane kwa maana ya kuomba au kusali. Hii ni kwa sababu katika dini ya Kikristo wakristo huyaona maombi kama hali ya kuzungumza na Mungu. Wanaamini kuwa wanapoomba Mungu huwajibu. Anasema hivi baada ya madai yake ya kwenda mbinguni yanapokosa kutimia.

3.2.5 Osha

Damu ni kitu kiowevu chenye rangi nyekundu kinachozunguka katika mishipa ya kiumbe na ni ya muhimu sana kwa uhai mwilini mwa binadamu. Ukosefu wa damu mwilini huonyesha kuwa kuna dalili za kutoweka kwa uhai wa mwanadamu. Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* Mama anamwambia Almasi yafuatayo, “Hakuna kuchelewa mno. Damu ya Yesu itakutosha na itakuosha utakate kama theluji” (uk.39).

Mama anamwambia Almasi maneno haya baada ya Almasi kumwambia kuwa anahisi ameharibika sana na kwamba hawezi kuwa kasisi. Damu ya Yesu katika muktadha huu ni ile ambayo Yesu aliimwaga msalabani aliposulubiwa. Wafuasi wa dini ya Kikristo wanaamini kuwa Yesu alisulubiwa msalabani kwa ajili ya dhambi za mwanadamu. Damu katika hali hii ina maana ya ndani. Wakristo wanaamini kuwa damu ya Yesu ina maana ya kusafisha na kutakasa ili kufanya maisha ya mwanadamu safi. Damu hii ina maana ya msamaha wa dhambi na kwamba ina uwezo wa kuosha na kuondoa maovu kwa wale wenye hiyo imani. Inasimamia msamaha na utakaso na wokovu. Aidha, inaaminika kuwa damu ya Yesu inawapa uhai wa kiroho na ushindi wa kukabiliana na hali ngumu katika maisha ya humu duniani ndio maana Mama anamwambia Almasi kuwa damu hiyo itamwosha hadi atakate kama theluji.

3.2.6 Kutembea na Yesu

Kutembea ni hali ya kwenda au kusonga kwa miguu. “Kutembea na Yesu” ni kirai chenye maana ya kutembea kwa miguu pamoja na Yesu. Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* Mama anamwambia Almasi maneno haya kama wosia anapokuwa mwanafunzi katika Shule ya upili ya St. Joseph. Hii inajitokeza mwandishi anaposema maneno yafuatayo, “Almasi alikuwa anafuata nasaha ya mamake ya kutembea na Yesu katika uwanja wa shule ya upili ya Mtakatifu Yosefu” (uk.39).

Mama anatumia maneno haya kama wosia kwa Almasi kipragmatiki. Maana inayorejelewa hapa si kutembea pamoja na Yesu bali kutii sheria zake kila anapokuwa shuleni. Tunaambiwa maneno haya kumrejelea Almasi wakati alikuwa ameamua

kuhudhuria mikutano ya “Christian Union” alipokuwa mwanafunzi katika Shule ya Upili ya St. Joseph.

3.2.7 Mungu ni mkubwa

Haya ni maneno ya Mama katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi*. Mama anayasema maneno haya baada ya mumewe Masasi kurejea nyumbani siku nyingi baada ya kutoweka kwake. Masasi alikuwa ametoweka nyumbani bila kuieleza familia yake alikoenda, jambo ambalo lilikuwa limemtia Mama wahka. Anaporejea nyumbani Mama anasema, “Nilijua Mungu atakuleta salama *musakhulu* (mzee)...Jamani Mungu ni mkubwa” (uk.161).

Maana ya kileksika ya neno mkubwa ni –enye kuzidi kwa umbo au kimo. Hii maana ya neno imepanuliwa kwa kiwango fulani kumaanisha –enye uwezo au mamlaka. Anaposema kuwa Mungu ni mkuu harejelei kimo chake bali ule uwezo alionao ambao umeweza kumshawishi mumewe kurejea nyumbani.

3.2.8 Mungu ameniambia

Neno ambia kisemantiki kumweleza mtu habari hasa kwa kutumia kinywa. Haya ni maneno ya Paulina baada ya madai yake kuwa ataenda mbinguni siku hiyo kugonga mwamba. Wakati watu wamekusanyika ili kushuhudia kwenda kwake anasema kuwa anaenda kuzungumza na Mungu. Anapotoka huko alikokwenda kushauriana na Mungu anasema, “Mungu ameniambia sifi leo. Kuna jambo la ajabu anataka nilione kwanza” (uk.114).

Baadhi ya wafuasi wa dini ya Kikristo huamini kuwa Mungu huzungumza nao kwa njia nyingi. Baadhi ya njia hizo ni kama vile kupitia sauti, ushawishi wa moyo, Biblia na kadhalika. Mama anaposema “Mungu ameniambia” ina maana ya kipragmatiki. Hii ni kutokana na ukweli kuwa wakristo wanaamini kuwa Mungu ni roho. Katika usemi wake ni bayana kuwa anamaanisha kuwa amepata ushawishi fulani katika moyo wake kuwa hafi leo; si kwamba amemwona Mungu mwenyewe akimzungumzia.

3.2.9 Ng’oa macho

Macho ni sehemu ya mwili ambayo hutumiwa kuona. Kung’oa ni neno lenye maana ya kileksika ya kuondoa kitu hasa kilichopandwa au kilichopigiliwa au kumea. Huu ni usemi uliodondolewa kutoka kwenye Biblia katika mafundisho ya Yesu. Kifungu hiki kimerejelewa na Masasi katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* baada ya kutangazia watu kuwa ameokoka. Anasema haya, “Sasa maandiko nasema kama macho yako mocha yaani nafanya wewe nafanya tambi, ng’oa. Yaani ona pila macho hio kapisa” (uk.147).

Katika kifungu hiki usemi ‘ng’oa macho’ umetumiwa kipragmatiki kuleta maana ya kuondolewa mbali na chochote ambacho kinakuingiza katika ushawishi wa kutenda dhambi licha ya mienendo mibaya kuwa na faida kwa mtu husika. Maana ya kawaida ya maneno haya kuondoa sehemu ya mwili inayoitwa macho imepanuliwa ili kuleta maana zaidi ambayo ni kubadilisha mienendo.

3.2.10 Kuona pila macho hio kapisa

Katika kifungu kilichonukuliwa hapo juu usemi huu pia umetumika kipragmatiki kumaanisha kuepuka mambo maovu katika ulimwengu licha ya kuwa yanamfaidi

mhusika kwa namna fulani ili kumpendeza Mungu. Kwa mfano, iwapo mtu ni mwizi ni afadhali auepuke wizi huo ili aingie katika ufalme wa mbinguni badala ya kuiba na kutajirika kisha kuishia kwenda jehanamu.

3.2.11 Kusafisha njia

Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* usemi huu hizi umetumika kipragmatiki. Usemi huu umedondolewa kwenye wosia wa Majisifu kwa kakake, Nasaba Bora aliyekuwa mfuasi wa dini ya Kikristo wakati huo. Wosia huu ulielekezwa kwa Mtemi Nasaba Bora aliyekuwa amejaribu kumchumbia msichana fulani waliyekuwa wakisafiri naye lakini hatimye aligundua kuwa alikuwa kilema. Kuptia maelezo ya mwandishi tunaambiwa yafuatayo:

Nasaba Bora alipomweleza mdogo wake juu ya kisa hicho Majisifu alimwambia kuwa lilikuwa somo kwake toka kwa muumba. Alipaswa kulikisi tanga lake na kusafisha njia zake ili apate maghufura ya Mwenyezi Mungu (uk.102).

Usemi “kusafisha njia” umetumiwa kipragmatiki bali si kileksika katika muktadha huu. Kusafisha ni kuondoa uchafu nayo njia ni mahali pa kupitia. Mwalimu Majisifu anapomwambia asafishe njia hamaanishi aondoe uchafu mahali pa kupitia. Maneno haya yamepanuliwa kimaana ili kuleta maana ya ziada mbali na ile ya kisemantiki. Kwa vile Nasaba Bora alikuwa amejaribu kujihusisha katika mapenzi ya kiholela, anashauriwa kwa maneno haya kwa maana ya kuwa alifaa ajiepushe na maovu ili akubalike na Mungu.

3.3 Kubanika kwa neno

Hii ni mbinu ya kufasiri lugha ya sajili ya dini ya Kikristo ambayo huhusu matumizi ya neno lenye maana pana kuonyesha maana finyu. Wamitila (2008) anasema kuwa hali hii hutokea pale ambapo maana ya neno hufinywa. Ufinyaji huu wa neno kimaana hutokea pale ambapo maana moja maalum ya neno inatawala na kuishia kufanya maana nyinginezo za neno husika kupotea au kufifia au labda kupotea kabisa. Mifano mingi ya semi zinazotumika katika sajili ya dini ya Kikristo zimebaniwa kimaana ili kuleta maana moja maalum.

Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kuna lugha inayodhihirisha sifa za sajili ya dini ya Kikristo. Katika sajili hii kuna maneno mbalimbali ambayo licha ya kuwa yana maana nyingi, maana hiyo imefinywa hivi kwamba inaleta maana moja maalum. Hatuna budi kufafanua baadhi ya maneno ambayo aghalabu hutumika katika muktadha wa dini ya Kikristo ili kudhihirisha maana finyu ilhali kwa kawaida yana maana pana. Miongoni mwa maneno haya ni pamoja na:

Ndugu

Baba

Bwana

Neno

Kukubalika

Malaika

3.3.1 Ndugu

Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* neno hili linatumiwa kumrejelea Masasi baada ya kutangaza ulokole wake hadharani. Hapo awali alikuwa akiitwa Masasi lakini baada ya kuokoka anaitwa “ndugu Masasi”. Maana ya neno ndugu imebanwa kuleta maana ya mtu unayeshiriki naye katika shughuli za dini. Maana nyingine za neno hili kama vile rafiki na jamaa zimepuuzwa.

3.3.2 Baba

Neno hili lina maana anuai kama vile: mzazi wa kiume, kaka wa baba, jina la heshima na kiongozi wa kanisa katoliki. Neno hili linapojitokeza katika usemi wa Mama linajitokeza na maana moja maalum. Wakati Mama anadai kuwa Mungu amemwita aende mbinguni anawaita wanawe na kuwaambia: “Naenda mbinguni kwa baba” (uk.110).

Ni bayana kuwa maana nyingine za neno hili zimepuuzwa. Licha ya kuwa na maana nyinginezo limetumiwa na Mama kuleta maana ya jina la heshima kwa maana ya kumrejelea Mungu. Kwa hivyo, limefinywa kimaana.

3.2.3 Bwana

Kileksika, neno hili lina maaana zaidi ya moja: jina la heshima la mwanamume, mume, mwanamume ambaye ni mwajiri, Mwenyezi Mungu au kihisishi cha kugutusha. Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* Mama anapolitumia neno hili maana hizi zote inaishia kubanwa hivi kwamba linasalia kuleta maana moja maalum. Anasema, “Wanangu mimi namshukuru Bwana mwokozi kwa kuwawezesha kuitika wito wangu mara moja” (uk.

109). Kwa mujibu wa usemi huu maana nyingine za neno baba imefinywa na kusaza maana moja tu: jina la heshima.

3.3.4 Neno

Neno hili linaweza kuwa na maana tofauti tofauti kileksika kama vile; mkusanyiko wa sauti, jambo la maana, jambo kubwa na balaa. Neno hili limejitokeza katika *Kidagaa Kimemwozea* kwa maana moja. Mwandishi anasema:

Ndani ya nyumba, Mtemi Nasaba Bora aliendelea kupaza sauti katika usomaji wake wa neno, hana mwao kuhusu mambo yatendekayo nje ya jumba lake lenye fahari (uk.103).

Mwandishi anasema maneno haya baada ya Mtemi Nasaba Bora kumwagiza mkewe amletee Biblia na kuanza kuisoma. “Neno” limefinywa kimaana katika muktadha huu na kubaki na maana moja tu ambayo ni “Biblia”.

3.3.5 Kukubalika

Kukubali ni hali ya kupokea wazo, ungama, ridhika, kiri, afiki, au toa ruhusa. Neno hili linajitokeza katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kama nukuu lililodondolewa kutoka kwenye Biblia. Kupitia mbinu rejeshi Nasaba Bora anakumbuka baadhi ya nukuu alizokuwa akiwanukulia hayati babake aliyekuwa kasisi. Mfano wa kifungu alichowasomea ni:

Petro akafungua kinywa chake akasema: Hakika nawaambia kuwa Mungu hana mapendeleo bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye. (uk.99)

Maana ya neno “hukubaliwa” katika nukuu hili imefinywa na kuleta maana moja maalum ambayo ni kupata kibali kwa Mungu. Maana hii inabainika hivi kwa vile kulingana na nukuu hili mtu hukubaliwa tu na Mungu baada ya kutenda haki.

3.3.6 Malaika

Hili ni neno lenye maana ya kiisimu ya kiumbe kichanga cha binadamu. Aidha, lina maana ya nywele zinazomea mwilini mwa binadamu au kiumbe cha kimbinguni chenye umbo la kibinadamu ambacho huwa na mbawa. Mzee Masasi anapookoka Mama anafurahi na kusema kuwa malaika juu mbinguni wanashangilia kwa vile nafsi moja imemkubali Mungu. Hii ina maana kuwa maana nyingine ya neno hili inafungiwa nje na kubakisha maana moja tu ambayo ni kiumbe cha kimbinguni.

3.4 Kukisia maana

Huu ni ukadiriaji wa hali. Ni aina ya ufasiri wa maana ya neno ambapo neno lenye maana finyu linapanuliwa kimaana ili kuhusisha maana ya kitu kinachohusiana nacho ambacho kina maana fulani tofauti na maana halisi ya neno kiisimu. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kwa mfano, Nasaba Bora anaamua kuwalakabu Imani na Amani majina kutoka kwenye Biblia (Amnoni na Tamara). Hali hii inamhitaji msomaji kukisia maana ya majina haya kwa kuwahusisha na tabia za watu wenye majina haya katika Biblia. Katika Biblia Amnoni alihusiana kimapenzi na dadake wa kuzaliwa. Hii ina maana kuwa lakabu hizi zinaashiria kuwa Imani na Amani wanahusiana kimapenzi.

3.5 Hitimisho

Kama ilivyodhihirika katika sura hii ni bayana kuwa semi nyingi zinazotumiwa na wafuasi wa dini ya Kikristo huwa na maana ya kipragmatiki. Wasikilizaji na wasomaji wa mazungumzo ya dini ya Kikristo hawana budi kutumia mikakati mbalimbali ili kufasiri semi hizo.

Ni bayana kuwa mazingira maalum ambamo neno fulani linatumiwa huathiri ufasiri wa msikilizaji wa neno hilo. Inakuwa vigumu kwa mzungumzaji ambaye hayuko katika mazingira hayo au kushiriki katika shughuli husika au tajriba fulani kuelewa maana inayokusudiwa. Muktadha ambamo neno limetumiwa huathiri ufasiri wa neno hilo. Kuna wataalamu ambao walibainisha aina mbili za miktadha ambazo humwezesha msomaji/msikilizaji kufasiri usemi fulani: muktadha wa kiisimu na muktadha wa hali halisi. Muktadha wa kiisimu unahusu matumizi ya matini au sentensi ambamo neno fulani limetumika kufasiri maana ya neno. Yule (1996) anasema kuwa muktadha wa kiisimu hudokeza maana za maneno kama inavyojitokeza katika muktadha wa maneno katika kipindi kimoja.

Muktadha halisi unahusu mazingira mahususi ambamo neno fulani limetumika. Katika sura hii tumetumia nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner kudhihirisha njia mbalimbali ambazo hutumiwa kufasiri maana ya semi za dini ya Kikristo. Wahubiri na washiriki wa dini ya Kikristo hutumia lugha iliyosheheni semi zenye maana kipragmatiki ili kufikia malengo mbalimbali.

SURA YA NNE

MCHANGO WA SAJILI YA DINI YA KIKRISTO KATIKA RIWAYA ZA

KIDAGAA KIMEMWOZEA NA NDOTO YA ALMASI

4.1 Utangulizi

Katika sura hii tulijikita katika kudhihirisha mchango wa sajili ya dini ya Kikristo katika kumwezesha mwandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kuyafikia malengo yake. Mwandishi wa riwaya hizi mbili amefaulu katika kuangazia sajili ya dini ya Kikristo. Hali hii bila shaka imefanikisha jitihada zake za kuwasilisha ujumbe wake katika jamii. Mtunzi yeyote yule wa kazi ya fasihi huwa na sababu ambayo huwa imemsukuma kuitunga kazi yake. Sababu hii hujitokeza wakati kazi husika imesomwa kwa makini. Wakati mtu anaisoma au kuisikiliza kazi yoyote ya fasihi kuna wazo ambalo hutawala katika kazi hiyo. Hili wazo ndilo humwezesha msomaji au msikilizaji kubaini lengo lililomfanya mwandishi kutunga kazi yake.

Mtunzi wa kazi ya fasihi hana budi kutumia mbinu mbalimbali katika kazi yake ili kuyafikia malengo yake. Malengo ya mtunzi wa kazi ya fasihi yanaweza kuwa pamoja na kuonya, kuelimisha, kukejeli mienendo hasi katika jamii, kuliwaza au kuchekesha.

Mtunzi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* ametumia sajili ya dini ya Kikristo katika kazi yake bila shaka ili kuyafikia malengo anuai. Mwandishi

amefanya hivi kwa kuwasawiri baadhi ya wahusika kwa namna kuwa wanajitokeza kama wafuasi wa dini ya Kikristo. Kupitia kwa wahusika hawa, amedhihirisha matumizi ya lugha ya kipekee katika kuyarejelea masuala ya dini ya Kikristo.

4.2 Maudhui

Kujitokeza kwa sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kumechangia katika kujenga maudhui kadha. Baadhi ya maudhui haya ni pamoja na dini, unafiki na mabadiliko.

4.2.1 Dini

Dini inaweza kuelezwa kama imani inayohusiana na mambo ya kiroho kwamba kuna muumba ambaye aliumba ulimwengu huu na kwamba ndiye mtawala wa kila kilichomo. Kuna aina nyingi za dini kama vile dini ya Kikristo, Kiislamu na Kibudha. Sajili ya dini ya Kikristo ndiyo inayodhihirika katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Hali hii inadhihirishwa na unukuzi wa vifungu kutoka kwenye Biblia na baadhi ya wahusika. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* tunaona wahusika fulani wakinukuu vifungu kutoka kwenye Biblia katika usemi wao. Kwa mfano, Mtemi Nasaba Bora anakumbuka jinsi babake mzazi aliyekuwa kasisi alivyokuwa akiwanukulia Biblia ili kuwaelekeza. Anasema, “Mungu hana mapendeleo bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye”. (uk.99).

Vilevile, katika *Ndoto ya Almasi* kuna wahusika wanaonukuu Biblia wanapozungumza na wahusika wenzao. Albina anapokuja kumuaga Mama Almasi ambaye anadai kuwa

amepokea wito wa kwenda mbinguni anamtuma na ujumbe ufuatao, “Mwambie Yesu tunaendelea kufanya ile kazi alituachia ya kugeuza maji kuwa divai” (uk.109). Licha ya kuwa kauli hii imenukuliwa kutoka kwenye Biblia ambapo Yesu alibadili maji kuwa divai, imetumiwa kwa njia ya kitashtiti kwa vile haimaanishi kuwa hiyo ndiyo kazi wanayoendelea kufanya ya kugeuza maji kuwa divai.

Katika mifano hii kuna unukuzi wa maandiko matakatifu kutoka kwenye Biblia. Hali hii inatoa ithibati ya kutosha kuwa kuna dini ya Kikristo katika jamii husika. Wahusika wanaonukuu vifungu hivi wamesawiriwa na mwandishi kama wafuasi wa dini ya Kikristo. Katika *Kidagaa Kimemwozea* babake Nasaba Bora anasawiriwa kama kasisi wa kanisa.

4.2.2 Unafiki

Unafiki ni kujaribu kudhihirisha sifa nzuri ambazo kwa hakika hana. Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kuna wahusika ambao wamejitokeza kama watu wanaotumia lugha ya dini ya Kikristo ili waonekane kuwa na sifa wasizokuwa nazo. Hawa ni wahusika ambao aghalabu wamewahangaisha watu na kuwatesa kisha wanakimbilia dini kama mahali pa usalama.

Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* tunamwona mhusika anayechangia pakubwa katika kuwepo kwa matatizo ya wanajamii. Mtemi Nasaba Bora ndiye kiongozi wa eneo la Sokomoko. Anatwaa uongozi huu baada ya ukoloni mkongwe. Pindi tu anaposhika hatamu ya uongozi uhuru walioutarajia wanasokomoko unaishia kuwa ndoto kubwa.

Nasaba Bora anawanyanya wananchi kwa kuwapokonya mashamba yao na kuwapangia wengine wao njama za kuuawa ili anyakue mali yao.

Uovu wake unapogunduliwa na wananchi anakimbilia dini. Tunaambiwa kuwa wanapokuwa wameketi katika kasri lao anamwambia mkewe amletee Biblia ambayo ilikuwa imejaa vumbi kwa muda mrefu. Mkewe anamletea Biblia ambayo anaanza kuisoma na kumwomba mkewe asikilize. Mwandishi anasema, “Bi. Zuhura anapojaribu kunyanyuka kwenda kutazama kuna nini mumewe kamwambia aketi kitako asikilize neno” (uk.102). Kauli hii inamdhihirisha Mtemi Nasaba Bora kama mnafiki kwani licha ya kuwa anasoma Biblia, anapuuza kilio cha DJ ambaye ameng’atwa na mbwa wake na baadaye kudai kuwa ilikuwa stahili yake.

4.2.3 Mabadiliko

Mabadiliko ni ile hali ya mambo kuwa tofauti na yalivyokuwa hapo awali. Kwa kawaida maudhui yoyote yale hukuzwa na viumbe wa mwandishi wanaoitwa wahusika. Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* ametumia sajili ya Kikristo kudhihirisha maudhui ya mabadiliko.

Katika riwaya ya *Ndtoto ya Almasi* Masasi ambaye hapo awali alikuwa mhusika aliyesawiriwa kama mlevi anabadilika na kuwa mlokole. Hapo awali alizungumza kwa sauti ya kilevi na kusema mambo yanayohusu pombe. Mhusika huyu anapobadilika mwandishi anamsawiri akitumia sajili ya dini ya Kikristo. Hali hii inaonyesha wazi mabadiliko ya kitabia ya mzee Masasi. Mathalan, tunamwona akinukuu vifungu kutoka

kwenye Biblia. Anatumia sajili ya dini ya Kikristo ambayo ni tofauti na ile aliyokuwa akitumia hapo awali. Anawahimiza wakazi wa Cherengani kuepuka vishawishi vya kutenda dhambi kama vile Biblia inasema (uk.147).

Katika *Kidagaa Kimemwozea* kuna mhusika mwingine anayebadilika. Mtemi Nasaba Bora ambaye hapo awali alikuwa mpyoro na katili anabadilika kwani tunaona akitumia lugha inayohusiana na dini ya Kikristo. Hii inajitokeza anapomwomba mkewe amletee Biblia na kuanza kuvisoma vifungu vya Biblia kwa sauti ya juu.

4.3 Ukuzaji wa dhamira

“Dhamira” ni neno lililowahi kutumiwa kwa maana ya lengo au kusudi la mwandishi.

Hata hivyo, kuna waliopinga fasili hii ya neno dhamira kwa madai kuwa ni muhali kujua lengo la mwandishi. Wamitila (2003) anasema yafuatayo kuhusu dhamira:

Mwandishi anapoanza kuandika riwaya au kazi yake huwa na lengo fulani. Msomaji huenda asiwe na bahati ya kukutana na msanii au mwandishi akamwuliza lengo au alichokusudia kusema katika kazi yake. Msomaji huyo atalazimika kuisoma riwaya hiyo kwa makini na kuangalia ni wazo gani analolikuza au kuliendeleza mwandishi katika riwaya yake kuanzia mwanzo hadi mwisho. Aghalabu lengo au wazo hilo ndilo huweza kuakisika kwenye anwani ya riwaya yake. Lengo hilo au wazo hilo ndilo linalojulikana kama dhamira. (uk.187)

Kwa jumla tunaweza kueleza dhamira kama kusudi la mwandishi kuiandika kazi yoyote ya fasihi. Lengo hili hujitokeza wazi baada ya msomaji kuisoma kazi husika kwa makini

huku akielewa maudhui pamoja na wahusika. Riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* ni kazi zinazohusu masuala ya kijamii kama vile siasa, utovu wa maadili na unafiki.

Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* wazo mojawapo linaloelekea kujitokeza ni kuonyesha mchango wa dini katika kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii. Katika riwaya hii Mama ni mhusika aliyesawiriwa kama mfuasi wa dini ya Kikristo. Jambo hili linadhihirika wazi kwani tunaona akitumia sajili ya dini ya Kikristo tangu mwanzo hadi mwisho wa riwaya ya *Ndoto ya Almasi*. Kwa mfano, usemi wa Mama umesheheni sajili ya dini ya Kikristo kila anapowaamkua wanawe.

Kupitia kauli mbalimbali zinazotolewa na Mama ni wazi kuwa yeye ni mcha Mungu kwani kila mara sajili ya dini ya Kikristo inadhihirika katika usemi wake. Hali hii ya Mama kuwa mlokole ndiyo inayomsababisha kudumu katika ndoa yake licha ya changamoto zinazomkumba katika ndoa hii. Mojawapo ya changamoto zinazomkumba mama katika ndoa yake ni ulevi na uasherati wa mumewe. Kuna wakati ambao Masasi (mumewe) anatoweka nyumbani bila kumjulisha anakokwenda. Almasi anapomuuliza Mama alikokwenda babake mama anasema, “Mungu akipenda mume wangu atarudi siku moja” (uk.154).

Kupitia huu usemi wa Mama ni dhahiri kuwa dini ndiyo inamsababisha Mama kuvumilia changamoto zinazomkumba katika ndoa likiwemo suala la uasherati wa mumewe. Mama

anaamini kuwa siku moja mume wake ataokolewa na kuwa mtu mwema licha ya mienendo mibovu ya sasa.

4.4 Ujenzi wa wahusika

Wahusika ni dhana inayoweza kuelezwa kama viumbe wa mwandishi. Wanaitwa viumbe wa mwandishi kwani hao hubuniwa na mwandishi. Mwandishi ndiye huamua hatima yao. Wamitila (2003) anasema yafuatayo kuhusu wahusika, “Wahusika ni viumbe au watendaji wanaopatikana katika kazi ya kifasihi. Viumbe hawa ni nguzo (mwega) mkuu wa dhamira” (uk. 211).

Kwa kawaida, wahusika wa fasihi andishi hufanana sana na binadamu katika maisha ya kawaida ingawa si lazima wadhibitiwe na kanuni zote za binadamu halisi. Mambo ambayo hudokeza sifa za wahusika ni pamoja na majina yao, maneno yao, maelezo ya mwandishi, maneno ya wahusika wengine kuwahusu, mitazamo yao na ushahidi na uchangamano wao.

Kupitia sajili ya dini ya Kikristo, mwandishi wa *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* amefaulu katika ujenzi wa wahusika wake. Yeye Mwandishi huwaumba wahusika na kuwaamulia hatima yao kama afanyavyo Mungu wa mbinguni. Miongoni mwa mambo yanayodhihirisha sifa za wahusika ni matendo yao, usemi wao na yale wanayosema.

Katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* mwandishi amefaulu kutumia sajili ya dini ya Kikristo katika kuwasawiri. Hii ni kwa sababu wamedhihirisha matumizi ya lugha yenye sifa za sajili ya dini ya Kikristo katika usemi wao. Kutokana na maneno yao yaliyokolea sajili ya dini ya Kikristo inakuwa rahisi kuuelewa msimamo wao katika maisha.

4.4.1 Mama

Mama ni mhusika wa kike ambaye ndiye mamake Almasi. Ana mume anayejulikana kama Masasi. Katika ndoa yao wamejaliwa kuwa na watoto watatu ambao kwa sasa wengine wao wameolewa. Hii inadhihirika wazi kuwa Mama amedumu katika ndoa yake kwa miaka mingi. Kupitia sajili ya dini ya Kikristo msomaji anaelewa sifa kadha za Mama.

Mama ni mhusika ambaye anadhihirisha sifa ya uchaji wa Mungu katika maongezi yake. Takriban kauli zote anazotoa mhusika huyu zinathibitisha kuwa anamheshimu na kumcha Mungu. Kwa mfano, anaimba nyimbo zinanoonyesha kuwa anamwabudu Mungu. Kwa mfano, anapimba wimbo unaoonyesha kuwa ana matumaini ya kufika mbinguni siku moja na kukutana na rafiki yake ambaye ni Yesu. Wimbo wenyewe unasema kuwa yeye hana rafiki mwingine humu duniani ila Yesu aliye mbinguni. (uk108)

Kupitia wimbo huu inadhihirika wazi kuwa Mama ni mcha Mungu kwa vile amemfanya Yesu kuwa rafiki yake katika maisha. Hii ina maana kuwa yu radhi kuyatii maagizo yote aliyopewa na Mungu ili asivunje uhusiano wake naye. Mama anatumia sajili ya dini ya Kikristo inayoonyesha kuwa ana matumaini yenye msingi katika Biblia. Katika sura

iliyopita tulikuwa tumesema kuwa sajili ya dini ya Kikristo husheheni matumaini. Wafuasi wa dini ya Kikristo huwa na matumaini kuhusu maisha mazuri baada ya kufa kwao. Tunaona kuwa Mama anakumbwa na matatizo mengi ya maisha kama vile umaskini na ulevi wa mumewe.

Mwandishi amemsawiri Mama kama mwenye heshima. Hii inajitokeza katika matumizi ya lugha ya dini ya Kikristo iliyosheheni heshima. Katika baadhi ya kauli zilizotolewa na Mama anadhihirisha heshima kwa Mungu. Aghalabu anatumia neno “baba” kumrejelea Mungu. Neno hili hutumiwa kama jina la heshima linalotumiwa na watu wa kawaida kuwarejelea wazazi wao wa kiume. Baadhi ya kauli alizotoa zinazodhihirisha sifa ya heshima ni zifuatazo, “Naenda mbinguni kwa baba” (uk.110).

Imani ni mambo anayokubali mtu kuwa ni ya kweli na anayopasa kuheshimu. Sajili ya dini ya Kikristo husheheni suala la imani kwa kiwango kikubwa. Jambo hili linatokana na ukweli kuwa mambo ya kidini hayawi ya kuonekana kwa hivyo mfuasi wa dini hulazimika tu kuamini kuwa yapo. Miongoni mwa kauli anazotoa Mama ni kama vile, “Mimi kile najua kwamba huko juu mbinguni shangwe ni tele kwa malaika mwenye dhambi mmoja anapotubu” (uk.147).

Mama anatoa kauli hii kama jibu kwa swali la Almasi kuhusu madai ya kuokoka kwa Masasi. Masasi ambaye amekuwa kafiri kwa miaka mingi walioishi na Mama katika ndoa sasa anadai kuwa yeye ni mlokole. Hata hivyo, vitendo anavyofanya kwa mujibu wa Almasi vimekithiri mipaka. Kwa mfano, anatengeneza mbawa kwa mbao na kufanya jitihada za kupaa kwazo hadi mbinguni. Jambo hili linadhihirisha kuwepo kwa imani

inayokithiri mipaka. Hata hivyo, Mama ana imani kuwa kuna sherehe za malaika kwa sababu ya wokovu juu mbinguni licha ya kuwa mumewe anafanya mambo yaliyokithiri mipaka.

4.4.2 Masasi

Masasi ni mhusika wa kiume ambaye ni mumewe Mama. Yeye amesawiriwa kama mhusika mwenye kupenda kulewa na mwasherati. Tangu mwanzo wa hadithi anadhihirisha tabia ya kutojali maslahi ya familia yake kwani kuna wakati anahama nyumbani kwa miezi kadha na kuenda kusikojulikana. Hata katikati ya hadithi tunaona kuwa anaacha kulewa kwa muda mrefu na kutangaza hadharani kuwa ameokoka. Punde si punde anabadili mtindo wake wa kutumia lugha kwani anaanza kutumia lugha ya dini ya Kikristo.

Masasi anadhihirisha sifa ya kumcha Mungu pindi tu anapotangaza kuwa ameokoka. Anaanza kumheshimu Mungu na kuwahubiria watu kuwa wanafaa kuyatii maagizo yake. Aidha, anaiwacha mienendo yake ya zamani ya kutenda maovu kama vile ulevi na uasherati. Mazungumzo yanajitokeza na unukuzi wa vifungu vya Biblia hali ambayo inamsawiri kama mcha Mungu. Kwa mfano, anasema:

Yeso Kristo yaani aliubiri kwa mulima mika silisopita yaani na mimi nafuata nyayo sake kwa kuubiri kutoka chuu ya ...ili yaani nyinyi watu wa Cherengani musikie. Sasa maandiko nasema kama macho yako mocha yaani nafanya wewe nafanya tambi, ng'oa. Yaani ona pila macho hio kapisa (uk.147).

Hali ya Masasi kudhihirisha sifa za sajili ya dini ya Kikristo katika usemi wake inamwezesha msomaji kumwelewa kama mwenye mcha Mungu. Anaamini kuwa mambo fulani ni ya kweli licha ya kuwa hajayashuhudia. Katika kuhubiri kwake ananukuu vifungu vya Biblia kama vile, “Unakumbuka yaani sauti ilitoka mbinguni Yesu alipofika katika mutoni Yortani, ehe, “Wewe ni mwanangu mpentwa: nimekukubali wewe” (uk.38).

Katika kifungu hiki cha Biblia alichonukuu Masasi kunayo mambo yanayoaminiwa na wakristo kuwa yalifanyika. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* pia mwandishi amefaulu katika kutumia sajili ya dini ya Kikristo kuwakuza wahusika wake kwa kina. Hali hii imejitokeza kupitia wahusika fulani wanaochorwa kwa namna wanayoitumia sajili hii katika mazungumzo yao. Wahusika ambao wanakuzwa kupitia kwa sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya hii ni Mtemi Nasaba Bora, Balozi na babake Nasaba Bora.

4.4.3 Mtemi Nasaba Bora

Hali ya Mtemi Nasaba Bora kusoma na kunukuu vifungu kutoka kwenye Biblia inamdhihirisha kama mnafiki. Hii ni kwa sababu yeye amekuwa kiongozi aliyewatesa na kuwanyanya watu aliowaongoza. Yeye yuko katika hali ya watu kumlaumu na kumlaani kufuatia maovu aliyowatendea kama vile wizi na ukatili ndipo anajitia kuwa msomaji wa Biblia. Tunamwona akimwagiza mkewe amletee Biblia iliyojaa vumbi kwa sababu ya kutosomwa kwa miongo kadha. Akiwa katika harakati za kuisoma anakataa kuitika wito wa mkewe wa kugharamia matibabu. DJ aliyeng’atwa na jibwa lake. Hali

hii inamchora kama mnaifiki anayejitahidi kujificha katika dini licha ya uovu aliowatendea watu.

4.4.4 Balozi

Huyu ni mhusika anayejitokeza katika uwanja wa Uhuru mnamo siku ya sherehe ya uzalendo. Yeye ndiye mfawidhi wa sherehe ya siku hiyo. Katika mazungumzo yake anadhihirisha sifa za sajili ya dini ya Kikristo. Anapowahutubia watu anasema yafuatayo kuhusu Mtemi Nasaba Bora:

Anatambulika kwa fadhili na utu wema wake, si katika eneo hili la Sokomoko tu bali katika Tomoko nzima. Kiongozi aliyeteuliwa na mwenyezi Mungu mwenyewe. Yeyote ajaribuye kumpinga anapingana na kudura za Mwenyezi Mungu. (uk.68)

Usemi huu unaodhihirisha sifa za sajili ya dini ya Kikristo unaoendelezwa na Balozi unamchora kama mdanganyifu. Anatumia dini ya Kikristo ili kuwafanya watu wamheshimu kiongozi asiyejali maslahi ya watu ambaye ni Mtemi Nasaba Bora.

4.4.5 Babake Nasaba Bora

Huyu ni mhusika ambaye hadithi inapoanza tayari ameaga dunia. Kupitia mbinu rejeshi tunaelezwa kwamba alikuwa kasisi aliyewahimiza wanawe kumcha Mungu. Mtemi Nasaba Bora anakumbuka siku zake za utotoni babake alipokuwa akiwanukulia vifungu vya Biblia ili kuwaasa walipokosea. Mfano wa kifungu anachokumbuka Nasaba Bora ni, “Petro akafungua kinywa chake akasema: Hakika nawaambia kuwa Mungu hana

mapendeleo bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye”
(uk.99).

Kifungu hiki miongoni mwa vifungu vingine alivyopenda kuwasomea wanawe vilimwezesha mwandishi kumsawiri kama mcha Mungu. Hii ni kwa sababu kupitia vifungu hivi anawahimiza wanawe wamche Mungu.

4.5 Kujenga uhalisia

Uhalisia ni ile hali ya kitu kuonekana kana kwamba ni cha kweli. Mwandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* amefaulu katika kutumia sajili ya dini ya Kikristo ili kuifanya kazi yake kuonekana halisi. Katika sura ya kwanza tulikuwa tumesema kuwa fasihi ni zao la jamii na mtunzi wa kazi yoyote ile ya kifasihi hana budi kuakisi miktadha mbalimbali ya kijamii katika kazi yake. Kazi yoyote ya kifasihi hutegemea lugha kama malighafi kuu ya kuwasilisha ujumbe. Kwa upande mwingine, jamii huathiri namna lugha hiyo itatumika katika miktadha mbalimbali.

Mtunzi wa fasihi hana budi kudhihirisha mitindo tofauti ya lugha anapoangazia miktadha mbalimbali ya kijamii. Mtunzi wa *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* amefaulu katika kuangazia miktadha halisi wa dini ya Kikristo kwa kutumia lugha ya kipekee anapoangazia masuala ya dini. Hali hii imeifanya kazi yake kuonekana halisi na kiwakilishi kamili cha mambo yanayojiri katika jamii husika.

4.6 Kuendeleza msuko

Msuko ni neno linalotumiwa kumaanisha ule mfuatano wa matukio katika kazi ya fasihi. Msuko hujengwa kwa maandishi na usemi wa viumbe wa mwandishi waitwao wahusika. Katika ile harakati ya kunukuu vifungu vya Biblia pamoja na matumizi ya mazungumzo yenye sifa za sajili ya dini ya Kikristo, mwandishi huendeleza msuko wa hadithi.

Mtunzi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* amefaulu katika kutumia sajili ya dini ya Kikristo kuendeleza msuko wa kazi zake. Kupitia wahusika wake, kuna mbazi zilizonukuliwa kutoka Biblia ambazo zimechangia katika ukuzaji wa msuko wa riwaya hizi. Mbazi ni hadithi za Biblia ambazo aghalabu huwa na maana iliyofumbwa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* Masasi ananukuu mbazi inayosema kuwa Yesu alisema kuwa ni heri mtu aziepuke hali zote ambazo huenda zikamfanya atende dhambi.

4.7 Hitimisho

Katika sura ya pili tulithibitisha kuwa mwandishi wa riwaya za *Kidaga Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* ametumia lugha ya kipekee kurejelea masuala yanayohusiana na dini ya Kikristo. Ken Walibora ametekeleza jambo hili kupitia maelezo yake mwenyewe pamoja na matendo na usemi wa wahusika. Ukweli ni kwamba mtunzi wa kazi hizi alikuwa na sababu ya kutumia lugha ya kipekee kurejelea masuala ya dini ya Kikristo. Kama tujavyo, fasihi ni aina ya sanaa kwa hivyo kila mtunzi wa kazi ya kifasihi hana budi kudhihirisha ufundi wa aina yake. Kwa sababu hii ni dhahiri kuwa kila kitu ambacho mtunzi hukisema katika kazi yake hutokana na jamii husika.

Mtunzi wa kazi yoyote ile ya kisanaa huakisi muktadha mahususi wa kijamii. Kwa mfano, kuna methali ambazo aghalabu hutumika katika maeneo ya Pwani. Hivyo basi, mtunzi wa kazi ya sanaa hana budi kubadili mitindo ya lugha anaporejelea hali na miktadha tofauti tofauti katika jamii. Katika sura hii tumethibitisha kuwa mtunzi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* amefaulu kutumia sajili ya dini ya Kikristo ili kuifanikisha kazi yake kwa njia nyingi. Baadhi ya njia hizi kama tulivyokwishaeleza awali ni kama vile kukuza dhamira pamoja na maudhui.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumejikita katika ufafanuzi wa matokeo ya utafiti wetu. Kwa kifupi tumejadili matokeo ya uchunguzi wetu kwa kurejelea sababu za uchunguzi huu pamoja na maswali ya utafiti wetu. Aidha, tumetoa hitimisho la utafiti wetu uliohusu udhihirikaji, uamilifu na ufasiri wa semi za sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*.

5.2 Muhtasari wa kazi

Tulidhamiria kuchambua riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kwa kuzingatia suala la sajili ya dini ya Kikristo. Ili kuyafikia malengo yetu ilitubidi kudurusu matini mbalimbali ambazo zilituwezesha kuifikia hatua hii. Aidha, ilitubidi tusome riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kwa kina ili tuweze kudondoa maneno na vifungu mbalimbali ili kuyatoa maelezo yenye uzito.

Malengo yetu ya utafiti yalikuwa kubainisha udhihirikaji wa sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Zaidi ya hayo, tulidhamiria kuonyesha mikakati ya kufasiri semi za sajili ya dini ya Kikristo kisha kuonyesha umuhimu wa sajili hii katika riwaya hizi. Tulijikita katika nadharia ya Blutner ya pragmatiki leksika ili kuonyesha fasiri za semi mbalimbali zinazohusiana na sajili ya dini ya Kikristo.

5.3 Hitimisho

Msukumo wa kazi yetu ulitokana na ukweli kuwa jamii huchangia pakubwa katika namna lugha inatumika katika jamii. Mukhwana (1990) anasema kuwa lugha haiwezi kutenganishwa na jamii, maana mahusiano ya jamii, anasema kuwa huchagua lugha fulani itumike mahali fulani. Kwa hivyo ni bayana kuwa wazungumzaji hutumia lugha kwa nia fulani. Mzungumzaji anapozungumza lugha huwa na lengo la kuwasiliana kikamilifu na wasikilizaji wake: yawe mazungumzo ya kisiasa, kiofisi, sokoni au ya kidini.

Lengo letu hasa lilikuwa kuchunguza mtindo wa lugha aliotumia mwandishi katika kurejelea suala la dini ya Kikristo. Katika uchunguzi huu imebainika kuwa sifa za sajili ya dini ya Kikristo zinadhihirika katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*. Pia tumedhihirisha ya kwamba mwandishi kupitia kwa sajili ya dini ya kikristo amefanikiwa kuuwasilisha ujumbe wake kidhabiti na kwa mtindo mwafaka unaoana na mazingira aliyoyamulika.

5.4 Mapendekezo

Uchunguzi wetu ulihusu udhihirikaji, umuhimu na ufasiri wa sajili ya dini ya Kikristo katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi* kwa kuegemea katika nadharia ya pragmatiki leksika. Tunawapendekezea wachunguzi wa baadaye kuhakiki namna waandishi wengine walivyosawiri masuala mbalimbali kwa kutumia sajili nyingine.

MAREJELEO

Binyanya, M. R. (2014) “Sajili ya Maafisa wa Polisi: tathmini ya Kiswahili katika Kituo cha Polisi cha Central” Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Bitinyu, H. M. (2011) “Nafasi ya dini katika ndoa: tathmini ya *Utengano na Paradiso*.” Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Blutner, R. (2011) *Some Perspectives on Lexical Pragmatics*, Pragmatics Reader. London: Routledge.

Crystal, D. (1969) *Language and Religion, 20th Century Catholicism*. New York, Hawthorn Books, U.S.A.

Grice, H.P. (1989) *Studies in The Way of Words*. Cambridge Mass: New York, Havard University Press.

Fishman, J.A. (1972) *Language in Sociocultural Change*. Standford: Standford University Press.

Habwe, J. Matei, A. na Nyonje, J. (2010) *Darubini ya Isimujamii*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M. A. and Hassan, R. (1976) *Cohesion in English*. London: Longman.

Halliday, M. A. (1974) *Language and social*. London: Longman.

Hills, D.P. (1997) *Preaching and communication*. The Army Chaplaincy Summer Fall.

Indede, F. (2007) “Lugha ya Kitamaduni ya Dini ya Kikristu” Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Maseno.

Ipara, I. na Maina, G. (2008) *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.

Iribemwangi, P.I na Mukhwana, A. (2011) *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers.

King'ei, K.G. (1992) "*Advanced Language Skills in Kiswahili*" Lecture Series, University of Nairobi.

Lawless, E.J. (1988) *The special Language of Pentecostalism*. University Press of Kentucky, U.S.A.

Mathooko, P. (2007) *Isimujamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njigua Books.

Mukhwana, A. (1990) "Siasa na Uimarikaji wa Kiswahili" Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutiso, K. (1996) "*Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry, Kasida ya Burudai*." , Nairobi University.

Nthenya, E. M. (2011) "Communication Strategies by Interpreters from selected Pentecostal Churches in Machakos Town, Kenya" Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Maseno University.

Okombo, L. (2011) "Sitiari, Taashira na Tashbiha katika Uwasilishaji wa Dhamira katika *Utenzi wa Tambuka: Uhakiki wa Kimtindo*", Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Okuku, W. M. (2010) "Uchanganuzi wa Kiisimu wa Baadhi ya Matini za Kiswahili Mtazamo wa Pragmatiki Leksika". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Rahim, A. (2012) “Language and Religion; Linguistic Religion or Religious Language”,
Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, TEFL, University of Kashan.

Walibora, K. (2006) *Ndoto ya Almasi*. Nairobi: Moran Publishers.

Walibora, K. (2011) *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Spotlight Publishers.

Wamitila, K.W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus
Publishers.

_____ (2008) *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa
Publishers.

Waweru, T. (2012) “Ubadilishaji Misimbo katika Kanisa la Katoliki”. Tasnifu ya Uzamili
ambayo haijachapishwa , Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Wilson, D. na Cartson, R. (2007) *Unitary Approach to Lexical Pragmatics: Relevance,
Inference and ad hoc Concepts*. Italy.

Yule, G. (1996) *The study of language. 2nd edition*. Cambridge: Cambridge University
Press.